

KONGAMANO

 Ketini. Nina furaha kuwa katika ninii, tumekusanyika katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, kusikia jumbe kutoka kwa Bwana, tukijua ya kwamba tunaishi tena katika siku za mwenendo wa Kanisa la kimitume. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya jambo hili!

² Leo imekuwa siku nzuri sana. Tumekuwa na mahojiano na watu, na kadhalika, na Roho wa Bwana amekuwa karibu, nasi tumeona mambo makuu yakitukia. Nami ninaamini ya kwamba tuko karibu na mwisho, karibu sana, karibu sana kuliko tunavyowazia hasa kwamba ndivyo tulivyo.

³ Kwa hiyo usiku wa leo ni usiku mwingine ambao tuna majaliwa ya, upande huu wa Umilele, kukusanyika pamoja kuna juu ya Neno Lake. Ninaamini kama tukifunga tu mkutano na kwenda nyumbani, ingetufaidi mara nyingi kuwa tu huku usiku wa leo, huu uimbaji, na kusikia mawaidha, na Roho akinena na watu.

⁴ Kuangalia katika Maandiko na kuyachunguza, hivi ndivyo i—ilivyoanza, hivi ndivyo itakavyoishia. Je, uliwahi kuona ya kwamba ufalme wa Mataifa ulianzishwa kwa lugha zisizojulikana na fasiri? Mfalme Nebkadreza, yale maandiko ya mkono kwenye ukuta, lugha zisizojulikana na fasiri. Unaondoka vivyo hivyo, wakati wa Mataifa.

Loo, lingekuwa ni jambo zuri sana kama tungalikuwa na majuma machache tungeweza kuchukua kuzungumza juu ya unabii, na kadhalika, ninii . . .

⁵ Nilimwuliza Ndugu Jack Moore, rafiki yangu wa thamani, leo kama ingekuwa ni sawa nikitangaza jambo fulani katika hili kusanyiko usiku wa leo. Kasema, “Hakika.”

⁶ Kuanzia Jumapili ijayo, juma moja, tarehe nne hadi kumi na moja, huko Jeffersonville, ninazungumza siku nane usiku huko juu ya *Nyakati Saba Za Mwisho Za Kanisa*. Nitaandika maelezo madogo juu yake, naye Bwana alionekana kuweka moyoni mwangu kwamba ningelinena mbele ya kanisa.

⁷ Nalo litaenda kwenye kanda ya sumaku, na kutoka hapo hadi kwenye santuri, na kutoka kwenye santuri hadi kwenye taipureta, hati mkato, kupiga chapa, na kisha yachapishwe ambayo yanafanya angalau vitabu vitatu vipya vinavyotolewa sasa vya maono, halafu kitabu hiki kitatolewa, *Nyakati Saba Za Mwisho Za Kanisa*. Ninaamini ya kwamba tuko katika wakati huo.

⁸ Kilichonifanya kukiandika, nilikuwa nikiangalia nyuma kila wakati Bwana anaposema nami ninaliandika, kisha

ninaliangalia, na kuliletea watu, na kuwaonyesha jinsi linavyotimia. Nilichukua unabii, sikuninii, nilikuwa mchungaji wa kanisa la Kibaptisti kule, hata sikujua maana ya ono, na sasa, mambo hayo yaliyotukia, ningeyaita, “kushikwa na njozi.” Sikujua kuliita ono, wakati huo, nilikuwa tu mvulana, 1933, mnamo Juni.

⁹ Nilikuwa nikienda zangu kwenye shule ya Jumapili, ndipo nilipokuwa nikichukua Biblia yangu ono likaja mbele yangu, nami nikasimamishwa sakafuni. Na hivi ndivyo lilivyosema, liko kwenye karatasi ya manjano, litachapishwa katika *Mbiu Ya Imani* moja kwa moja, kwa sababu karibu yote yametimia. 1933, wazieni jambo hili sasa, miaka mingi, mingi iliyopita, yapata miaka ishirini na minane iliyopita li—lilitukia, angalieni jinsi Neno Lake lilivyo sahihi.

¹⁰ Kasema, “Sasa tuna rais, Bw. Roosevelt, na huyu Bw. Roosevelt ataufanya ulimwengu uingie katika vita vya ulimwengu kupitia ninii yake, katika kipindi chake cha utawala kama rais.”

¹¹ Na kisha kasema, “Na katika wakati huu wamewaruhusu wanawake kupiga kura, ambalo litakuwa ni laana kwa taifa, watamchagua mtu asiye faa wakati mmoja.” Nao walifanya hivyo hivi majuzi. Naam. Sasa, wazieni hilo.

¹² Kasema, “Tutaingia vitani na Ujerumani, nayo Ujerumani italindwa nyuma ya zege, nasi tutapigwa vita vibaya sana mahali hapa,” Ngome ya Maginot, miaka kumi na mmoja kabla haijajengwa. Mnaona? Kweli kabisa.

¹³ Kasema, “Mtawala huyu mpya wa mabavu, Mussolini, atapiga hatua yake ya kwanza kuelekea Ethiopia, nayo Ethiopia itaanguka miguuni pake.” Ilianguka. Ilisema, “Hilo litakuwa la mwisho kwake, ataishia katika aibu.”

¹⁴ Nami nikasema, “Itakuwa kabla ya wakati wa mwisho kuja kwamba kutakuwako na mwanamke mashuhuri atakayesimama Marekani, kwa sababu Marekani imetiwa alama kama mwanamke, namba yake ni kumi na tatu, naye atasimama, ama awe rais, au,” nikayaweka kwenye mabano, “(labda huyo mwanamke, kwa kuwa alikuwa ni mrembo na anavutia, atakuwa ni kanisa Katoliki) lakini katili moyoni, naye atalielekeza taifa kwenye upotovu.

¹⁵ “Na ndipo itakuwa kwamba magari yataboreshwa kufikia mahali, ambapo niliona familia moja ikiendesha motokaa iliyokuwa na paa la kioo, wala haikuwa na usukani ndani yake.” Ilikuwa... Nami niliona hivi majuzi ya kwamba, katika *Makanika Pendwa* kwamba mtambo huo tayari umevumbuliwa, wanaweza kulipeleka popote utakapo kwa namna fulani ya ninii, udhibiti huu wa rada. Lifanyie tu maandalizi, nalo linaenda moja kwa moja. Hata hulihitaji, na limefunikwa na kioo.

¹⁶ Ndipo nikageuka kuangalia nami nikaona Marekani ilikuwa ikifoka moshi, kitu fulani kilikuwa kimeiteteza.

¹⁷ Na chini pale nikasema, “Si katika njozi, bali, ninabashiri,” kumbukeni hili, nadhani hili linarekodiwa, pia, “Ninabashiri ya kwamba mambo haya yatatukia kati ya sasa, 1933, na 1977.” Ambayo itatupa miaka kumi na sita zaidi kama ubashiri wangu ukitimia kikamilifu.

¹⁸ Sasa, kulikuwa na mambo saba yaliyonenwa ambayo yangetukia, matano ya hayo tayari yametukia, kuna mawili yaliyosalia kutukia. Itakuwa hivyo. Hiyo ni kusema, katika Jina la Bwana itakuwa hivyo. Mnaona?

Loo, Yeye ni mkuu, na... [Mtu fulani ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹ ...Baba, kwa Roho Zako, kwa ajili ya... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...tuma juu ya watu, karama zilizomo Kanisani. Tunakushukuru, Bwana, kwa kuwa wanazungumza kwa umoja, wananena katika umoja kuhusu kuja Kwako. Manabii, wenye kunena kwa lugha, wafasiri, wote wanatuonya, wakati umewadia, na kwa kweli tunaamini ya kwamba wakati umeenda kuliko tunavyodhania. Jalia tuiandae mioyo yetu na nafsi zetu kwa ajili ya kuja kwa Bwana.

²⁰ Na, usiku wa leo, tunaposoma katika Neno Lako, naomba unene nasi sasa kupitia Neno lililoandikwa. Tunaomba, katika Jina la Yesu, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

²¹ Katika Kitabu cha Isaya kwa ajili tu ya Ujumbe mfupi, ili nisiwaweke muda mrefu kupita kiasi. Ninataka kuliambia kusanyiko ambalo halikuwa hapa asubuhi ya leo, najua wengi wenu iliwabidi kufanya kazi, ni vibaya kuwa na mkutano siku ambayo watu hawana budi kufanya kazi.

²² Lakini ndugu yetu mwema na mpendwa, rabi, alitupa ujumbe mzuri sana juu ya wa—wakati na juu ya Biblia. Nami bila shaka nimeufurahia u—ushirika ambao ndugu yetu amekuwa nao pamoja nasi hapa, na ule nimekuwa nao pamoja naye. Naye hana budi kuondoka usiku wa leo saa tano *na kitu*, na alisema itambidi kuondoka yapata saa nne na nusu. Nikasema, “Labda tutakuwa tumemaliza kufikia wakati huo.” Nami hakika ninamthamini sana. Mungu na amfanikishe, ndilo ombi langu.

²³ Wengi wenu mlisikia unabii mdogo uliotolewa si muda mrefu uliopita katika kanisa hili, na maskini mwanamke Mbaptisti; ulitimia jana usiku. Kwa hiyo nina hakika kanisa linajua kile tunachozungumzia. Kanisa hili usiku wa leo linasimama kwenye tukio la Mlima wa Kugeuka Sura. Ndivyo ilivyo.

²⁴ Hebu na tufungue Isaya mlango wa kwanza, na tusome kutoka kifungu cha 17 na cha 18, labda cha 16 pia, tunaposoma:

*Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu
usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya;*

Jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu, wasaidieni walioonewa, mpatieni yatima haki yake, mteteeni mjane.

Haya, njoni sasa, tusemezane, asema BWANA: dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu.

25 Baba, libariki Neno Lako Takatifu. Tunamngojea, Bwana, Roho Mtakatifu kutufunulia mambo haya. Nena na kila moyo kama tulivyo na haja, Bwana. Unasihi kupitia karama nyingi na kupitia Neno Lako, ukisihi katika barabara kuu na njia za kando, ukijaribu kuwashurutisha watu hawa wa saa kumi na moja kujiweka tayari, Wewe unakuja. Tujalie, Bwana, na unisaidie sasa, na unene. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

26 Kama ningeliita somo, ningetaka kuchukua somo la *Kongamano*, kwa sababu nilipokuja huku, niliona pale juu mlangoni panaitwa Mkutano wa Ushirika, na mkutano wa ushirika ni kama tu wakati ambapo tunafanya ushirika pamoja. Na sasa, wengi wenu mnamkumbuka yule mtu mzee na—na mpendwa, na mtumishi wa Mungu anayeitwa F. F. Bosworth, alikuwa mwenzangu na ndugu mpendwa, ambaye hivi majuzi tu alienda Nyumbani, akikaribia umri wa miaka mia moja, kukutana na Bwana.

27 Naye daima alikuwa na ucheshi mwingi, na wakati ningeikutana naye na kuzungumza naye, sikuzote angekuwa na ucheshi mdogo. Naye alizoea kusema, “Ndugu Branham, unajua *ushirika* ni nini?”

Nami nikasema, “Nafikiri najua, Ndugu Bosworth.”

Akasema, “Ni jamaa wawili katika meli moja.” Kwa hiyo, nafikiri huo ni usemi mzuri sana.

28 Sasa, alipokuwa akifa, mlisikia habari za kifo chake, bila shaka, nami nikakimbia upesi kwenda Miami kumwona. Basi nikaingia haraka mlangoni, na hapo akainuka, nikamwona akiinuka, na hizo nywele nyeupe na maskini kichwa chake chenye upara, akaninyoshea maskini mikono yake myembamba. Nikakimbia na kumkumbatia shingoni, nikapiga mayowe, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake!” Kwa kuwa kama kulikuwa na mtu ambaye ninamjua mwenyewe ambaye aliliongezea heshima kanisa la Kipentekoste, alikuwa F. F. Bosworth, mtu mashuhuri wa imani.

Ndipo akaniambia, akasema, “Ndugu Branham, nina neno kwa ajili yako, nami nina furaha sana ulifika hapa kabla sijaondoka.”

Nikasema, “Ni kitu gani?”

29 Akasema, “Harakisha uende kwenye huduma za kimishenari mara moja.” Kasema, “Hapo ndipo palipo na mafanikio katika

kazi ya Bwana kwa ajili yako.” Kasema, “Nenda, kabla baadhi ya vijana hawa hawajaenda na kuharibu njia ya kupitia.”

³⁰ Ndipo nikasema, “Ndugu Bosworth, ninataka kukuuliza swali, ndugu yangu mtakatifu wa thamani. Katika nyakati zote za huduma yako, ni wakati gani uliokuwa mzuri kuliko zote? Ulipompokea Roho Mtakatifu; au wakati mtu fulani alipoponywa; ama . . .?”

Akasema, “Sasa hivi ndilo tukio kuu sana nililopata kuwa nalo maishani mwangu mwote.”

Nikasema, “Hivi unatambua unakufa?”

³¹ Akasema, “Yote ambayo nimeishia, kwa zaidi ya miaka hamsini, Ndugu Branham, ni Yesu Kristo,” naye akasema, “dakika yoyote Yeye anaweza kuingia mlangoni kunipeleka Nyumbani.”

³² Wakati mauti yalipompiga, alisimama chumbani na kupeana mikono na watu kwa zaidi ya saa mbili, waongofu wake, na baadhi yao walikuwa wameondoka kwa miaka hamsini.

Ninaipenda hiyo *Zaburi Ya Maisha*, sehemu yake inasema:

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha

Nasi tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu.

Kumbukumbu ambazo labda mwingine,
Huku akisafiri kwenye bahari kuu ya maisha,
Ndugu mpweke aliyeharibikiwa na meli,
Akiona, atatiwa moyo tena.

Naipenda hiyo.

³³ Tunakutana pamoja kujadili mambo. Tumesikia mengi sana kuhusu makongamano siku hizi, kila kitu mnachosikia siku hizi kimekuwa ni kongamano. Wanafanya . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Makongamano ya UN kote ulimwenguni.

³⁴ *Kongamano* ni nini, kwa vyovyote vile? Ni la nini? Ni la wakati biashara, ama wakuu wa mashirika wanapokusanyika pamoja na kujaribu kutatua jambo bora kuliko yote wajuavyo.

³⁵ Wakati, kwa kawaida kongamano huitwa wakati wa hatari. Katika wakati wa hatari wanaita watu wao wenye akili kuliko wote, watu wanaonekana wanajua kuliko wote, nao wanawaleta watu hawa pamoja, viongozi wa mataifa, viongozi wa mashirika, viongozi wa makampuni ya biashara. Wakati kukiwa na hatari, wanawakusanya watu hawa pamoja, nao wanaketi chini na kutumia kilicho bora sana walicho nacho kulitolea hoja jambo hilo.

³⁶ Halafu tunaona ya kwamba tulikuwa na moja wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, ninaamini waliliita Ko—Kongamano

la Mabingwa Wanne; imekuwa ni miaka michache iliyopita, chini ya ishirini, ambapo walikuwa na Kongamano la Mabingwa Wanne. Wengi wenu ninyi wanaume na wanawake hapa mnaweza kukumbuka kongamano hilo, wakati ulimwengu mzima ulipokuwa katika wakati wa hatari, ulimwengu wa mashariki na wa magharibi ulikuwa umefikia mwisho mmoja kwa mwingine. Ujerumani, na mataifa ya Kinazi, na kadhalika, waliwaita pamoja watu wa—wao walio na akili kuliko wote, watu mashuhuri wa taifa, walio bora kuliko wote, na kuketi chini.

³⁷ Ninamkumbuka rafiki, rafiki yangu mhubiri, ndugu Mbaptisti, mtu mzuri sana, Dk. Pettigrew, huko Louisville, Kentucky, naye alikuwa akisikiliza taarifa rasmi ya kongamano hilo. Basi akasema ya kwamba alikuwa, alikuwa amefungua redio yake akisikiliza kutoka mahali ambapo taarifa zilikuwa zikiingia, kile walichokuwa wakijaribu kuamua.

³⁸ Nami nafikiri hivyo ndivyo sote tunavyopaswa kufanya, nafikiri wakati mambo yanapofikia mwisho, hatupaswi tu kuwa tukisikiliza, tunapaswa kuwa tukiomba, tukiwaombea viongozi wa taifa letu, tukiwaombea watu walio mamlakani, kwamba Mungu atatawala.

³⁹ Nilikuwa katika moja yao hivi majuzi nilipoona tulikuwa watu kumi na mmoja tumeketi mezani, kwenye ma—ma—mahakama kuu ya shirikisho, na mwishoni mwa hiyo meza kulikuwa na kiti kimoja kitupu. Nilihusika katika hili, nami ninajua ni Nani aliyekuwa ameketi pale jinsi lilivyoishia, Bwana wangu. Loo, nina furaha sana kwamba maombi hubadilisha mambo! Ndipo tulipokuwa...

⁴⁰ Dk. Pettigrew alisema alikuwa akitembea sakafuni akisikiliza hiyo taarifa rasmi, ndipo akasema mtu fulani alibisha mlangoni, na alikuwa ni mmoja wa aina hii ya watu walio wapinga-maadili mamboleo, wanaovaa ovaroli, na kusuka hiyo nywele ndefu, chini na juu, nanyi mwajua, wala sijui mimi, namna hizo zote za mambo ya kipumbavu naye akasema, “Nataka uende nami katikati ya mji, mimi—mimi huandika vitabu,” naye akasema, “ushairi, nami... Hawata—hawatanunua mashairi yangu,” kasema, “na—nawe ni mtu mwenye ushawishi,” tena kasema, “wewe—wewe njoo unisaidie na unipe mapendekezo.”

Naye akasema, “Mtu wangu mwema, ninasikiliza taarifa rasmi ya kongamano la wale Mabingwa Wanne. Ninataka kujua matokeo yake.”

⁴¹ Naye mpinga-maadili huyu akasema, “Loo, mashairi yangu, nyimbo zangu na roki ya kisasa,” ama bugi-bugi, vyovyote ilivyokuwa siku hizo, walivyokuwa wakifanya vijana, “ni muhimu zaidi kuliko hilo!” Bila kujua kama hilo lisingeenda sawa, kusingekuwa na taifa la kuwa na bugi-bugi tena, ama—

ama chochote wanachouita huo upuuzi. Sasa, loo, tunapaswa kuyajali mambo haya.

⁴² Kulikuwako na kongamano lingine lililoitwa Kongamano la Geneva, na, hapo ilipotubidi kuungana tena na mataifa, na kujaribu kutatua ni nini lililo bora zaidi kufanya; na kulikuwa na moja hivi majuzi tu lililoitwa Kongamano la Paris. Nao kwa kawaida huchagua mahali, mahali pazuri panapofaa.

⁴³ Hivi majuzi tu nilikuwa huko Geneva ambako walifanyia kongamano hilo, na inaonekana kuwa ni mahali ambapo wanaweza kuangalia nje na kuona vitu vinavyowatia moyo. Ni ajabu wakati—wakati mkazo unapokuwa juu ya mtu, hana budi kuwa na kitu cha kumtia moyo. Washairi hupanda juu milimani kutazama kuchomoza kwa juu; wengi huwa na kibanda huko nje mahali fulani; manabii wanaishi nyikani mbali na watu, mahali fulani kupata *kitu* kinachowavuvia.

⁴⁴ Nalo Kongamano la Geneva lilifanyika mahali pazuri, Kongamano la Paris, na kadhalika. Na kwa kuwa makongamano haya ya mataifa yanafaa sana, nasi tuna mengi sana. Nasi sote tunajua habari zake, tunasoma habari zao kwenye gazeti, na kusikia habari zao kwenye redio, na televisheni, na vituo vingine zaidi tulivyo navyo.

⁴⁵ Nasi tunajua habari zao, lakini hebu tuwazie baadhi ya makongamano ambayo Mungu alikuwa nayo. Mungu ana makongamano, pia. Yeye alisema hapa, “Njoni, tusemezane, asema Bwana, dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama sufu; nyekundu kama bendera, nyeupe kama theluji. Njoni, tusemezane.” Mungu anataka kongamano; Mungu ana makongamano.

⁴⁶ Katika makongamano ya ulimwengu watu hukutana pamoja na kula, kunywa, kudanganyana. Ni tofauti sana wakati Mungu anapofanya kongamano: Watu hukutana pamoja na kufunga na kuomba, wanapata maagizo kutoka Mbinguni, na kusonga mbele. Hebu tuzungumze juu ya moja ya makongamano ya Mungu, ama machache yake.

⁴⁷ Moja ya kongamano la kwanza nililoweza kuwazia Mungu akifanya lilikuwa ni lile kongamano la Edeni. Mungu alikuwa na kongamano huko Edeni. Wakati habari ilipoingia Utukufuni ya kwamba mwanawe alikuwa amepotea, kwamba alikuwa ametenda dhambi na kumpa kisogo Mungu wake, habari hizo zilifika Mbinguni. Hapana shaka ila ambapo, wengi wa Malaika walitaka kushuka waone kama wangeweza kufanya jambo fulani kulihusu, bali Mungu alitaka kufanya kongamano hilo Mwenyewe. Mtoto Wake ndiye aliyekuwa katika shida, asingeweza kumtumainia Malaika, lilikuwa ni kongamano muhimu.

⁴⁸ Na katika siku hii wakati wanatheolojia wanahubiri, nao watu wanasema ya kwamba Yesu alikuwa ni mwanadamu tu,

ya kwamba Yesu alikuwa ni nabii tu wa—wa kawaida, kwamba Yeye hakuwa Mungu, mbona ingeharibu picha nzima! Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii, alikuwa ni Mungu aliyeshuka katika mwili kufanya kongamano na upatanisho, hakuwa tu ni mtu wa kawaida ama nabii, Yeye alikuwa ni Mungu wa manabii, Naye akashuka katika mwili.

⁴⁹ Na wakati, hakika, bila shaka inaonyesha hilo hapo mwanzo, kongamano la kwanza ambalo Mungu alifanya na mwanadamu, Yeye alikuja Mwenyewe, hakulitumainia mtu mwingine. Wakati Mungu aliposhuka kumkomboa mwanadamu, Yeye kamwe hakulitumainia nabii, Yeye alikuja Mwenyewe, kwa kuwa Ndiye pekee ambaye angeweza kufanya hivyo.

⁵⁰ Na wakati kongamano hili kuu huko Edeni, Mungu alishuka, na, angalia tabia ya mwanadamu, inaonyesha jambo hilo leo katika mwanadamu, badala ya mwanadamu kujaribu kutoka, na kusema, “Bwana, nimetenda dhambi,” yeye hujificha mahali fulani. Na mara nyingi, kama vile Adamu alivyofanya, anajifanyia dini ya majani ya mtini, kitu fulani alichojibunia mwenyewe, namna fulani ya kanuni ya imani ambayo angetamka, na kujificha.

⁵¹ Lakini kama tu ilivyotukia kwa Adamu ndivyo itakavyokuwa kwa kila mtu ambaye ametumainia kanuni za imani. Kutakuwako na wakati utakaposimama karibu na Mungu, ambapo kanuni yako ya imani na dini yako ya jani la mtini haitaficha dhambi yako. Mungu alifanya njia, njia iliyoandaliwa.

⁵² Kabla hajaweza kuzungumza na Adamu, Yeye asingeweza kuzungumza naye akiwa uchi, ndipo akaua kitu fulani, kitu fulani hakina budi kufa, na kitu fulani kweli kilikufa kufanya kifuniko ili tuweze kufanya kongamano hili pamoja na Mungu. Hapana shaka Mungu alichagua mti fulani katika bustani ya Edeni, naye akawaita Adamu na Hawa, na kuzitupa hizo ngozi za kondoo za kale zilizolowa damu mle ndani, na kusema, “Vaeni hizi hapa nje.” Ni kongamano la jinsi gani!

⁵³ Basi wakati kongamano linapofanywa, kuna maamuzi yanayofanywa. Ndipo sisi ambao tunapokea uamuzi wetu hatuna budi kutenda ipasavyo. Mungu alifanya kongamano na Adamu na Hawa na kufanya uamuzi, kwamba ilikuwa ni damu, kwamba ilikuwa ni tiba ya Mungu, na kamwe haiwezi kubadilika. Hakuna kanisa, hakuna kanuni ya imani, hakuna mwanadamu, hakuna Malaika, hakuna ibilisi, hakuna kitu kingine chochote kinachoweza kuubadilisha huo. Mungu alifanya njia Yake iliyoandaliwa kwa mwenye dhambi kusimama katika Uwepo Wake, hiyo ilikuwa ni kwa damu iliyomwagika ya mtu asiye na hatia.

⁵⁴ Nasi sote tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo. Tusingeweza

kujiokoa wenyewe kwa kanuni zetu za imani, na kadhalika, kuliko vile tungeliweza kushika kamba zetu za buti na kuruka juu ya mwezi. Tumepotea, wala hakuna mmoja wetu anayeweza kumwokoia mwingine, hakuna mtu, hakuna nabii, hakuna kuhani, inamchukua Yesu Kristo, Ambaye alikuwa Mungu katika mwili, kutuokoa, Naye amefanya Dhabihu.

⁵⁵ Ninamwona amesimama pale, Adamu na mwili wake mkubwa wa kiume ambao ulikuwa ni sura kamili ya afya. Nilipokuwa Ugiriki hapa si muda mrefu uliopita, niliona pi—picha ya mtu asiyeongoka, msanii mashuhuri aliyekuwa amechora picha ya Adamu na Hawa. Ilikuwa ni kuwavunjia heshima wanadamu. Hawa alionekana kama mnyama, badala ya mama, nywele kubwa zikining'inia upande mmoja, na kinywa chake kimeenda kombo, na mguu mmoja mkubwa kuliko huo mwingine, na loo, alionekana wa kuchukiza mno. Hiyo ndiyo dhana ya akili isiyoongoka.

⁵⁶ Hawa alikuwa ndiye mwanamke mrembo kuliko wote aliyepata kutembea juu ya uso wa dunia, Yeye alimfanya. Macho yake yalikuwa kama nyota mbinguni. Nami ninamwona amesimama pale amezungushiwa ngozi ya kondoo iliyojaa damu. Mungu alikuwa akionyesha hapo kwenye kongamano hili jinsi mpango Wake ulivyokuwa kwa ajili ya wokovu wa siku za usoni wa ulimwengu mzima. Mwangelie Adamu wakati akiondoka, maskini hizo ngozi za kondoo zilizolowa damu zikipigapiga kwenye miguu yake mikubwa, ya kiume, na ya mke walipokuwa wakiondoka Uweponi Mwake.

⁵⁷ Ilikuwa ni kielelezo tu cha picha ambapo tungeweza kukielekezea kamera yetu sasa kwenye asubuhi moja huko Yerusalemu. Ninaweza kusikiliza nje ya dirisha na kusikia kelele. Ni kitu gani? Ni kasisi akisema, “Mwondoeni mtu kama huyo!”

⁵⁸ Ninaweza kumsikia maskini mwanamke mmoja akikimbia mbele ya umati, na kusema, “Kwani amefanya nini, ila kuwafunya wagonjwa, na kuwafufua wafu, na kuleta kufunguliwa kwa hao waliokuwa kifungoni?”

Mkono mkubwa katili ungempiga kofi mdomoni, useme, “Hivi ungensikiliza mwanamke huyo badala ya kuhani wako?”

⁵⁹ Mjeledi katili wa Kirumi ukimcharaza. Kidogo ni picha mbaya sana, lakini hebu tuinue mapazia tuangalie. Ninasikia kitu fulani kikigongagonga barabarani, juu ya mawe ya kutandaza chini, ninachungulia dirishani, nami nikamwona Mtu mdogo mwenye joho jeupe, lililosukwa kote bila mshono, limewekwa mabegani Mwake, amebeba msalaba wa kale huku ukigongagonga, akishuka kwenda barabarani. Mabega Yake yanachubuka, na kama nilivyoona kwenye maskini vazi Lake limejaa madoa madogo kila mahali, na madoa hayo, wakati akipanda kilima, yanakuwa makubwa zaidi na zaidi, baada ya

kitambo kidogo yote yanaungana kuwa moja. Sasa mtapakao mkubwa wa damu kwenye miguu Yake. Ilikuwa ni kitu gani? Adamu huyo wa pili, yule Mzao wa mwanamke.

⁶⁰ Nyuki wa mauti akivuma kukizunguka kichwa Chake anapopanda kile kilima, akijua ya kwamba punde tu ibilisi alikuwa, bila shaka, amemhadaa pale.

⁶¹ Ibilisi alisema, “Angewezaje mtu anayedai kuwa Mungu, angewezaje...? Nilimpa changamoto afanye sarakasi, au moja ya vitimbi vyake mbele zangu kugeuza mkate kuwa, au, mawe kuwa mkate, akashindwa kufanya hivyo. Angewezaje kusimama, kama yeye ni Nabii, na kumwacha askari wa Kirumi amfunge kitambaa usoni mwake, na kumpiga kichwani kwa fimbo, kisha kasema, ‘Sasa, kama wewe ni nabii tuambie ni nani aliyekupiga,’ na atulie? Yeye ni mwongo. Nitakuja nimchome kwa mwiba wangu wa mauti. Nitampata sasa!”

⁶² Loo, jinsi alivyoshindwa! Walipomtundika msalabani, naye nyuki huyo alikuwa akivuma karibu Naye... Kama nyuki, ama mdudu aliye na mwiba kamwe akiama na kuuchomelea mwiba huo kwa kilindi, akiondoka hawezi kuuma tena, anauacha huo mwiba wake mwilini. Mauti yangeweza kumchoma mwenye dhambi na kuepuka, lakini wakati huo aliuacha mwiba wake katika mwili wa Imanueli, Naye akauchomoa huo mwiba.

⁶³ Si ajabu Mtakatifu Paulo angeweza kusema miaka mingi baadaye wakati nyuki wa mauti alipokuwa akivuma karibu naye, “Ee mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, Yeye atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

⁶⁴ Mauti yalishindwa, nyuki anaweza kuvuma kote, nyuki wa mauti anaweza kuvuma, na kusema, “Nimekupata,” lakini tunaweza kuelekeza kidole huko kwenye kaburi tupu, na kusema, “Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

⁶⁵ Anaweza kupiga kelele, bali hawezi kukuuma, hana mwiba mwingine. Wakati alipochomelea mwiba wake katika mwili wa Imanueli, mwili wa Mungu miongoni mwetu, mwiba wa mauti uling’olewa. Hilo lilikuwa ndilo wazo la Mungu kwenye kongamano Lake la kwanza.

⁶⁶ Mwanadamu hana budi kuishi, si kwa nafsi yake; hapaswi kuja na nadharia yake mwenyewe ya kujibunia, Yeye aliihukumu; asingeweza kuja na kanuni ya imani ya kujibunia, ilimbidi kupitia njia iliyoandaliwa na Mungu. Kongamano liliamua, hayo yalitoshia, ilikwisha. Mwanadamu hana budi kuja kwa dhabihu.

⁶⁷ Hebu tuzungumze juu ya kongamano lingine kwa muda kidogo tu, kulikuwako na kongamano lingine, mengi ya hayo tungeweza kuyawazia, bali nitagusia tu mawili ama matatu, hapa, kwa dakika chache. Hebu tuwazie juu ya lile—ya lile—

Kongamano la Kichaka Kilichowaka Moto, wakati mmoja kulikuwa na Kongamano la Kichaka Kilichowaka Moto. Watu wa Mungu walikuwa wamepelekwa huko Misri.

⁶⁸ Na hapo tunajua jinsi Yusufu alivyouzwa, mfano mkamilifu wa Kristo, na jinsi ambavyo tulimwona akimwondosha kila Mmataifa kutoka karibu naye apate kujitambulisha kwa ndugu zake. Picha nzuri sana ya siku tunayoishi, wakati Injili inapowarudia Israeli tena, Yesu atajitambulisha kwa Myahudi mbali na Mmataifa.

⁶⁹ Ndipo tunapoonza ya kwamba baada ya miaka mia nne ya utumwa (Nao Wamisri wakainuka huko juu, na kulikuwako na farao ambaye hakumjua Yusufu, na hatimaye, wakafika mahali walipofanywa watumike kwa hali ngumu. Jinsi Wamisri walivyowafanya watumwa, na kuwapiga, na kuwasukuma kama wanyama!) Mungu aliwainulia nabii. Nabii huyo akatoroka, akamwoa msichana mrembo wa Kushi, naye akapata mwana, Gershomu, naye aliridhika sana kurithi pesa nyingi sana kutoka kwa baba yake, Yethro, ama, baba mkwe wake, Yethro. Naye alikuwa akiyachunga makundi yake upande wa nyuma ya jangwa, wakati kwa ghafla vilio vya watu wa Mungu vilipokuja mbele Zake. Ilibidi jambo fulani lifanyiike, Mungu alikumbuka.

⁷⁰ Nina furaha sana Yeye hukumbuka. Alikumbuka agano Lake, akakumbuka Edeni, akamkumbuka Ibrahimu, Yeye hukumbuka kila Neno alilowahi kuahidi, kila kitu alichowahi kusema, Yeye ni Mungu asiye na kikomo. Alikumbuka yote, Naye akakumbuka alitoa ahadi Yake.

⁷¹ Kuna jambo moja tu la Mungu kufanya, hilo ni kutimiza Neno Lake. Na kutimiza Neno Lake Yeye alikuwa amemchagua nabii, lakini nabii huyu alikuwa mtoro, huko nje nyikani, alikuwa mtoro, alikuwa ameenda nyikani, naye alikuwa ametulia. Lakini Mungu anapomchagua mtu kufanya jambo fulani, haidhuru anatoroka jinsi gani. . .

⁷² Mungu alikusudia kungekuwa na Kanisa katika siku za mwisho, pepo wanaweza kuinuka, na pepo, na wanafiki, bali Mungu atakuwa na Kanisa hilo, kwa sababu alisema litakuwako, Atafanya hivyo. Hakuna kitu kitakacho. . . “Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

⁷³ Ndipo wakati alipomwona huyu mtoro Wake, huyu nabii Musa, huko nje ameridhika sana na mke mrembo na familia, na anaelekea kuwa tajiri, moyo huo wa Kiyahudi, hiyo ilikuwa nzuri vya kutosha kwake, mzigo ulikuwa umemwondokea, kwa sababu alikuwa ameshindwa katika theolojia yake na katika elimu yake kuwakomboa wana wa Israeli, lakini Mungu alikuwa ameagiza kwamba afanye hivyo.

⁷⁴ Na kila kitu ambacho Mungu amekusudia kitatimia. Mungu atakuwa na Kanisa, Yeye atakuwa na watu, atakuwa na mtu wa kuamini karama Zake, atakuwa na wale watakaonena kwa

lugha, wale watakaofasiri, atakuwa na manabii, na Yeye—Yeye atafanya hivyo, kwa sababu alisema atafanya hivyo. Mungu atakuwa na uponyaji na wokovu, na Roho Mtakatifu atashuka, Naye anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.

⁷⁵ Sisi, Wabaptisti, Wamethodisti, Wapresbiteri, na kadhalika, tunaweza kuukataa kadiri tutakavyo, lakini Mungu atakuwa na Kanisa hilo hakika tu kama Neno Lake lilivyosema, atakuwa nalo. Yeye hukumbuka kila Neno alilosema, katika majira litakalozaa.

⁷⁶ Kulikuwako na Musa, ameridhika, tayari kukaa kule chini, lakini Mungu aliwazia, “Sina budi kufanya kongamano pamoja na nabii huyo.” Kwa hiyo akachagua mahali fulani. Hebu tuwazie palikuwa chini ya kichaka kingine, juu ya mlima. Mungu alipaa, akashuka kutoka Mbinguni na kukiwasha kile kichaka moto, ndipo akamwita Musa kwenye kongamano. Musa katika udhaifu wake akaanza kusihi, lakini alipouona utukufu wa Mungu, alikuwa tayari kwenda.

⁷⁷ Wakati mwingine watu wa Mungu wanapoitwa katika kongamano pamoja na Mungu, ambapo wanakutana na Mungu, mwajua, unalo nyumbani kwako wakati mtoto mchanga anapofikia mahali hata daktari anatoka, na kusema, “Hakuna—hakuna nafasi kwake kuishi,” mchungaji wako anasema, “Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu,” loo, hilo halilikomeshi, uko tayari kwa ajili ya kongamano, nawe ni mtu tofauti unapozungumza na Mungu.

⁷⁸ Unapokuwa na mvulana mpotovu, ama msichana mpotovu nawe unaweza kuomba kufikia mahali fulani, mpaka umlete Mungu jukwaani, ambapo Yeye atakutana nawe huko chini kwenye chumba cha kulala, huko nje kwenye banda, huko chini kwenye kitalu, popote pale, unapokuwa na kongamano hilo pamoja na Mungu, umebadilishwa, jambo fulani lilitukia. Nao watu walio na makongamano hayo pamoja na Mungu, na kukutana nao, wanakutana na Mungu, wanatenda kipumbavu kwa walimwengu baada ya hapo.

⁷⁹ Angalia ni picha ya kipumbavu jinsi gani, ilivyoonekana kwa Musa. Hapa lilikuwepo jeshi kubwa huko chini Misri, kama Urusi sasa, lilikuwa limeushinda ulimwengu mzima, Misri iliushinda, na huyu hapa mzee, mwenye umri wa miaka themanini, masharubu yamemfikia moja kwa moja mpaka kiunoni, nywele zenye mvi zikining’inia mgongoni mwake, umri wa miaka themanini, kesho yake asubuhi alikuwa amemketisha mkewe kwa kutagaa juu ya nyumbu na mtoto mdogo chini ya mkono wake namna *hiyo*, fimbo ya kale, iliyopinda mkononi mwake, akishuka, akimsifu Mungu kwa nguvu awezavyo kwenda.

Kasema, “Musa, unaenda wapi?”

⁸⁰ “Ninashuka kwenda Misri kuiteka.” Ni upumbavu jinsi gani! Jinsi ilivyoonekana kwa moyo usioongoka! Kitu gani? Alikuwa na...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...Mungu. Mungu alikuagiza kufanya hivyo. Haidhuru linaonekana la kipumbavu jinsi gani, Mungu atalifanya, kwa vyovyote vile.

⁸¹ Jinsi ilivyo kwa mwanamume au mwanamke Mpentekoste, huenda wakanena kwa lugha, huenda wakakimbia huku wameinua mikono yao, huenda wakafanya ming’ao ya kila namna, na hata wakati mwingine wanafikiri ni walevi ama wendawazimu, lakini wamekuwa na kongamano. Haidhuru lilionekana kwa ulimwengu, Mungu alilifanya, kwa vyovyote vile, kwa hiyo haijalishi.

⁸² Hivi hawakusema kwenye Siku ya Pentekoste, “Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya”?

Petro akasema, “Sivyo walivyo, vilabu bado havijafunguliwa, lakini *hili ni lile*.”

Vema, ndugu, mara nyingi nimetoa tamshi hili: “Kama *hili* silo *lile*, ninataka kuweka *hili* mpaka *lile* litakapokuja.” *Hili ni lile*.

⁸³ Halafu basi, kama ukiangalia, Musa akienda zake Misri, uvamizi wa mtu mmoja, lakini alifanya hivyo kwa sababu alikuwa amefanya kongamano pamoja na Mungu. Naye Mungu alikuwa amemwagiza, na kumwonyesha utukufu Wake, wala hakuna hata taifa lingeweza kumzuia. Mungu anapokutana na mwanadamu katika kongamano, na kumjaza na Roho Mtakatifu, na kuitia moto nafsi yake, hakuna kitu kitakachomzuia, anashuka kwenda kuteka.

⁸⁴ Wana wa Israeli walipokuwa wakirudi, walikuwa na kongamano lingine pamoja na Mungu, Musa alikuwa nalo kwenye Bahari ya Shamu, tutaliita hilo Kongamano la Bahari ya Shamu, wakati moja kwa moja kwenye jukumu lao kulikuwa na shida.

⁸⁵ Basi sikilizeni Wakristo, hapo ndipo mtakapofanya kosa lenu baya sana. Hapo ndipo Israeli ilifanya kosa lake baya sana, wakati walipoomba wapewe sheria ya kumtumikia Mungu. Katika Kutoka 19, baada ya neema kutoa mwokozi, Musa, nabii, alikuwa tayari amemtoa mwana-kondoo, alikuwa ameandaa agano, tayari ameweka mambo haya yote, na hata hivyo walitaka jambo fulani la kufanya wao wenyewe, walitaka theolojia fulani.

⁸⁶ Hiyo ndiyo shida siku hizi. Laiti tungaliiacha Pentekoste jinsi ilivyokuwa hapo mwanzo! Lakini ilitubidi kuwa na jambo la kubishania, ilibidi tuwe wa Umoja, Uwili, Utatu, Church of God, tungali, loo, jamani! Huku kupanda kwote kwa ngamia wenye nundu wa nundu moja, nundu mbili, nundu tatu, na kadhalika. Inaleta tofauti gani, kwamba ngamia ana nundu ngapi, maadamu tumempanda? Inaleta tofauti gani, kama uko kwenye Ford ama Chevrolet? Endelea tu kusonga mbele.

⁸⁷ Lakini ilitubidi kuwa na dhehebu, ilibidi tuwe na kutoka, mwajua. Ilitubidi kuwa na, mlango wa 20 wa—wa Kutoka naamini pale ambapo walikuwa wamepewa sheria, ilitubidi kuwa na kitu ambacho tungeweza kufanya kuonyesha ya kwamba tulikuwa Dk., Ph.D., LL.D., L. maradufu D. *Fulani-wa-fulani*, mnaona, kuwafanya waonekane kama walimwengu wengine.

⁸⁸ Kama vile Israeli walivyofanya kosa lao baya tena wakati walipomkataa Samweli, nabii, na kumtaka Sauli, Mfalme. Samweli akawavuta, akasema, “Je, nimewahi kuchukua yoyote ya pesa zenu? Je, nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ila lile Mungu aliloliunga mkono?”

⁸⁹ Hawangeweza kusema lolote, kasema, “Naam, hujachukua chakula chetu wala pesa zetu, na kila kitu ulichosema ni sahihi, bali tungali tunataka mfalme. Tunataka kuwa kama walimwengu wengine, kama mataifa ya Mataifa.” Wanaye.

⁹⁰ Hivyo ndivyo tunavyofanya. Hatuwezi kuacha baraka jinsi tu zilivyo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kwa kila mtu.

⁹¹ Hatuna budi kusema, “Sasa, sisi ni wafuasi wa kanisa *hili*; sisi ni wafuasi wa kanisa *hili*,” kutenda kama hao wengine. Pentekoste si dhehebu, wala haiwezi kuundiwa madhehebu, Pentekoste ni tukio la, “Yeyote atakaye na aje, apate kunywa Maji ya Bwana.” Ni tukio, Roho Mtakatifu akiishi ndani ya Wamethodisti, Wabaptisti, Wayahudi, na kadhalika, waongofu, na Wakatoliki, na wowote wale. Ni tukio tunalopitia tunapofanya kongamano na Mungu, kulizungumzia pamoja Naye.

⁹² Kwa hiyo wakaja kwenye wajibu wao, moja kwa moja kuikabili Bahari ya Shamu iliyofunga njia yao. Kwa kawaida unapokuwa na kongamano na Mungu, na kuanza kufanya jambo fulani, ibilisi hulizuia. Atakufanya mgonjwa sana usiweze kuamka, atamfanya kila jirani aongee juu yako na kukuita mtakatifu anayejibingirisha, atafanya jambo fulani kulihusu, na kukwambia unashuka kwenda kule uwe wa mtindo wa kale.

⁹³ Acha nywele zako zikue, yeye, “Utakuwa—utakuwa mtu wa kale, mshamba. Wasichana uliokuwa ukicheza karata nao hawatawazia wewe ni mrembo kama ulivyokuwa.”

⁹⁴ Hiyo inaleta tofauti gani? Hebu fanya kongamano na Mungu, nawe utaacha kucheza karata, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

⁹⁵ Lakini sisi, mnaona, tu—tunataka kuwa kama watu wengine, tunataka kutenda kama akina Jones. Tunajilinganisha, hebu paka vipandio vyako rangi nyekundu, na uangalie majirani wakipaka vyao rangi nyekundu. Hebu nunua Chevrolet na kuijivunia, mwangalie jirani yako akiondolea mbali Ford yake upesi sana. Hana budi kutenda tu kama wewe utendavyo,

unaona, huna budi kutenda kama yeye. Unataka kulinganisha matukio.

⁹⁶ Mara nyingi nimesema sijali kama suruali yangu inalingana na koti langu, tai yangu inalingana na shati langu, ninataka ujuzi wangu ulingane na Biblia ya Mungu. Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kufanya. Walichofanya wakati *huo*, hivyo ndivyo ninavyotaka *sasa*. Kwa nini uchukue kabadala wakati anga za Kipentekoste zimejaa yaliyo halisi? Kwa nini uchukue kitu ambacho hakikuwa sahihi? Chukua yaliyo halisi, kwa sababu Mungu yuko tayari kumwaga ninii Yake. . . “Ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu.” Ninahubiri juu ya hilo kesho usiku, Bwana akipenda, “Kwa yeyote atakaye na aje.”

⁹⁷ Na moja kwa moja kwenye wajibu wenu mtakabiliwa na kizuizi. Loo, nadhani maumbile yote yalitetemeka tu. Mbona, angalieni ni kitu gani, huyu hapa Musa na Israeli moja kwa moja kwenye wajibu wao huku Nguzo ya Moto ikiwaongoza, na kuwaelekeza moja kwa moja kwenye mtego.

⁹⁸ Mungu anapenda kuwaingiza watu Wake katika mitego, aone watakalofanya. “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa kwanza na kurudiwa.” Anawapeleka kule. Anakuleta hapa, anakuweka katikati ya maoni, “Sasa, hiyo inaweza kuwa ni telepathia ya kiakili? Yaweza kuwa...?” Unaona? Anakuweka kwenye mtego, aone ni uamuzi wa aina gani utakaofanya. Hiyo ni kweli. “Yachunguzeni Maandiko,” Yesu alisema, “Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Hiyo ni kweli. Sasa, Mungu huiacha iwe hivyo.

⁹⁹ Sasa, Yeye aliwaingiza Israeli moja kwa moja kwenye mtego, milima na majangwa pande zote mbili, jeshi la Farao likifuatilia, maelfu ya magari ya farasi na mikuki. Na kundi la maskini watumwa wanyenyekevu, maskini, wasio na silaha, walioshuka kwenye Bahari ya Chumvi, ama Bahari ya Shamu, hasa, moja kwa moja kwenye kingo zake, na haya hapa mavumbi ya magari ya farasi yakija, na hii hapa milima pande zote mbili, hakuna njia, ilionekana kana kwamba Mungu alikuwa ni Mwanajeshi duni, amewaacha watu Wake bila njia ya kurudi.

¹⁰⁰ Wakati mwingine Yeye hufanya hivyo, Anamwacha daktari aondoke, na kusema, “Hutaishi, utakufa. Hiyo kansa itakuua. Kamwe hutaamka kutoka kwenye kiti hicho.” Yeye, inaonekana kana kwamba anakuacha bila njia ya kurudi nyuma, bali Yeye ndiye kimbilio lako, angukia mikononi Mwake. Ee Mungu!

¹⁰¹ Yeye ni Kimbilio langu, Yeye ni Ngome yangu Kuu. “Jina la Bwana ni Ngome Kuu, wenye haki huikimbilia, wakawa salama.” Ngome za kimbilio. Yeye ndiye Kimbilio letu. Sina kimbilio lingine ila Yeye, sitaki kujua kimbilio lingine lolote, Yeye ndiye Kimbilio langu. “Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu; Ki—Kimbilio wakati wa dhoruba.”

¹⁰² Nakumbuka mara ya kwanza niliyopata kunena kwa lugha, nilikuwa nikihubiri kwenye Kanisa la Kibaptisti la Milltown, nami nilikuwa huko nje nikihubiri, nami nilikuwa nimemalizia kabisa, huku Wabaptisti hao wote wameketi pale wakiniangalia, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yangu, nami nikaruka katikati ya marefu ya kanisa na kuanza kunena kwa lugha. Nikawazia, “Vema, kwani ni nini kinatokea sasa?” Kamwe sikujua lolote kulihusu, halafu nilipoanza kurudi nikasikia midomo yangu ikisema hivi: “Mimi ndimi Mwamba katika nchi yenye uchovu, Ngome, uh, Kimbilio katika wakati wa dhoruba.”

¹⁰³ Loo, jinsi nilivyoshangaa! Na kila mmoja akiangaliana na mwenzake kama bata bukini uani, akiangalia *hivyo*, nami nilijisikia vivyo hivyo, maana sikujua, lakini najua jambo fulani lilikuwa limetukia ndani yangu. Loo, nilipata Ngome, Mahali pa Kujificha. Sijawahi kutaka kitu kingine chochote tangu wakati huo, ila mahali hapo, Mahali hapo pa Kujificha palipobarikiwa.

¹⁰⁴ Moja kwa moja kwenye wajibu, moja kwa moja chini ya moto wa adui, hao hapo. Ilionekana kana kwamba maumbile yote yalikuwa yakitetemeka kwa ajili yao. Ni saa ngapi? Utaratibu wa Kikristo ni—ni upi? Jambo la kufanya ni lipi katika wakati kama huo? Fanya kongamano. Hiyo ni kweli. Wakati kanisa linapofikia mahali ambapo *hili* linafanya *vile*, nalo *hili* linafanya *hivi*, na kila kitu kimepinduka, usiondoke kanisani, fanya kongamano, fanya mkutano wa maombi mahali fulani.

¹⁰⁵ Musa alichagua mahali, ningesema, hebu tuwazie palikuwa papo hapo nyuma ya ule Mwamba, akafika pale, na kusema, “Bwana Mungu,” kitu kama hiki, “Bwana Mungu, Yehova Mkuu, Yeye aliyekutana nami katika kichaka kilichowaka moto, tukio hilo halijawahi kuniacha, nami nimefanya kila kitu ulichoniambia nifanye, ninasimama kwenye wajibu, nimewaleta watu Wako hapa kama ulivyosema. Huko imening’inia ile Nguzo ya Moto, pale limesimama jeshi la Farao, hii hapa milima na Bahari ya Chumvi. Nifanye nini, Bwana? Je, inanibidi kujisalimisha kwa Farao? Nifanye nini? Ninakutaka Wewe.”

¹⁰⁶ Ninaweza kuona Malaika wakianza kuketi juu ya kila mwamba, pande zote. Loo, ni kongamano la jinsi gani! Baada ya kitambo kidogo Roho wa Bwana . . . ninaweza kuona Nguzo hiyo ya Moto ikisogea. Ilikuwa ni kitu gani? Kulikuwa na uamuzi uliofanywa. “Utafanya nini? Kusalimu amri, kurudi nyuma na kujaribu tena? Kurudi katika madhehebu, na ulimwengu?” La, bwana. Akasema . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁰⁷ Mungu kamwe harudi nyuma. Kamwe hawaambii watu Wake warudi kwenye yale Moody aliyosema, yale Sankey aliyosema, yale Finney aliyosema. Songa mbele! Amina.

¹⁰⁸ Shida yake siku hizi, sayansi itamwona Mungu kabla hatujamwona. Wanafanya uchunguzi katika milki, na wamevumbua vibaini uongo, na kadhalika, nao wanaweza

kuthibitisha kwamba kuna nguvu fulani. Mliona hivi majuzi katika—katika gazeti la *Look*... la, ilikuwa katika *Reader's Digest*, naamini, ambapo walimchukua mponyaji, na huko chini, ilikuwa huko Uingereza, waliyafungulia makanisa kile walichoita mponyaji, na yapata asilimia themanini zaidi ya watu waliponywa kuliko dawa ilivyopata kuwaponya huko Uingereza.

¹⁰⁹ Hiyo ilikuwa ni *Newsweek*, Gene, ama ilikuwa ni ipi? Unakumbuka? *Reader's Digest*. Vema. Walimchukua mponyaji waone kama kulikuwa na kitu chochote kilichotoka kwake. Wakaweka mkono wake chini ya eksirei, wakamwacha aombe, wakaweka kipande cha jaribosi waone kama ilikuwa ni mkono wake tu, ama kama kulikuwa na nguvu fulani... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹¹⁰ Hebu tuone yale Sankey aliyosema juu yake, yale Moody aliyosema, yale Knox, Calvin, ama mtu mwingine aliyosema kulihusu. Hilo ni sawa. Walikuwa—walikuwa ni watu wa Mungu katika siku hiyo, bali sisi tunasonga mbele. Sayansi inaweza tu kwenda *umba*... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?...

¹¹¹ “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Yeyote yule, na iwe. Rasilimali zisizotumiwa bado!

Mtu mmoja alisema si muda mrefu uliopita, kasema, “Si—sitaki kumsumbua Mungu, mwajua, na—najua Yeye ana shughuli nyingi sana.”

Upuuzi.

“Si—sitaki kuninii...”

¹¹² Vema, huwezi kumaliza wingi wa baraka Zake. Ungeweza kuwazia samaki mdogo mwenye urefu wa kama nusu inchi, huko nje katikati ya Bahari ya Pasifiki akisema, “Afadhali ninywe maji haya kwa unyimifu, maana huenda nikaishiwa?”

¹¹³ Ungeweza kuwazia maskini panya mdogo yapata *ukubwa-huu* chini ya maghala makubwa ya Misri akisema, “Afadhali nile, nijigawie punje mbili tu kwa siku msimu huu wa baridi kali, huenda nikaishiwa kabla ya mavuno mapya?”

¹¹⁴ Hiyo ni dhahaka. Vema, ni dhahaka hivyo maradufu, mara elfu moja zaidi, kuwazia unaweza kumaliza rehema za Mungu mwenye rehema. Mbona, Yeye anajaribu kujilazimisha aingie ndani yako. “Ombeni kwa wingi ili furaha yenu itimie.” Hakuna njia ya kummaliza.

¹¹⁵ Kama vile pampu, jinsi unavyozidi kusukuma, ndivyo maji yanavyozidi kuwa matamu. Loo, napenda hilo! Endelea tu kusukuma. “Kuishi kwenye mkondo ambapo Utukufu unatoka.” Napenda hilo.

¹¹⁶ Sasa, Musa alimlilia Bwana, naye Bwana akasema, “Simama uende mbele.” Ndipo Musa alipoenda moja kwa moja na kuingiza mguu wake majini, wakati hilo lilipotukia, Bahari ya Shamu ilifunguka, nao Israeli wakavuka wakapata ushindi mkuu; walikuwa na kongamano. Hivyo ndivyo inavyotubidi kufanya sikuzote, ni kufanya makongamano.

¹¹⁷ Sasa, ninataka kuzungumza juu ya lingine upesi sana. Kulikuwa na kongamano, kuna mengi ya hayo tungeweza kuzungumzia, lakini hebu tusilipite hili, kulikuwako na Kongamano la Gethsemane wakati mmoja. Wakati, ilibidi liletwe baada ya maisha ya ushindi kushinda maradhi, yakashinda kila kitu ulimwenguni, alikuja Gethsemane, na ilimbidi Baba kuchunguza kuona kama kweli alitaka kuipitia au la.

¹¹⁸ Wakati alipowaongoza wanafunzi Wake, nao wote wakashikwa na usingizi, nao wakajilaza chini na kulala usingizi, bali Yesu akaendelea mbele kidogo tu. Yeye hufanya hivyo daima, unaenda tu sehemu ya njia, na kumwangalia akienda mbele kidogo, kote kote, Yeye yuko mbele yako wakati wote, akitengeneza njia. Akaenda mbele kidogo tu, ndipo alipofika huko nje, akapiga magoti kando ya mwamba.

¹¹⁹ Hebu na tuwazie tu, ninaweza kumwona Gabrieli akishuka, upanga Wake mkuu ukisimama kando Yake, ninaweza kumwona Pakanga, ninaweza kuwaona Malaika hao wengine wakuu wakiangaza juu ya miamba pande zote. Ilikuwa ni kitu gani? Meza ya kongamano ikiandaliwa.

¹²⁰ Ndipo Roho Mtakatifu wa Mungu, kama tunavyoona kwenye picha ya Gethsemane, ile Nuru, ambapo Mungu ni Nuru, El, Elohimu, Yule aishiye Peke yake, wakati aliposhuka akaja katika Uwepo Wake, “Unataka kupitia yote, Mwanangu?” Ati nini? Malaika wanasikiliza. Matokeo yatakuwa nini? “Ulimwengu mzima uko begani Mwako. Je, unataka kulipia gharama, ama unataka kufanya nini? Unaweza kuja moja kwa moja sasa bila mauti. Hiyo hapo Kalvari mbele Zako, hapo watakutemea mate usoni Mwako, kisha watakupeleka Kalvari, mambo haya yote, utakufa kwa uchungu na taji ya miiba kichwani Mwako, na Damu Yako itatoka. Je, uko tayari?”

¹²¹ Hebu tuone kile kongamano hilo, mwangwi utakuwaje? Malaika wote wamesimama karibu, wakishangaa, “Ni nini kinatendeka sasa?”

¹²² Uamuzi umetolewa. Ni kitu gani? “Si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke.” Loo, Malaika wakafunua baraka zao, na kuanza kumhudumia wakati huo, wakimtayarisha kwa ajili ya saa hiyo kuu. Kongamano likaandaliwa, uamuzi ukafanywa, ninafurahia sana uamuzi huo.

¹²³ Uamuzi wangu mdogo, usio na maana, kama nitamtumikia au la unawezaje...? Rafiki mwenye dhambi, wako ungekuwaje—

uamuzi wako ungekuwaje usiku wa leo, Mungu, akibisha moyoni mwako wakati uamuzi kama huo ulipofanywa kwa ajili yako? Jibu lako ni lipi kwa mwaliko Wake? “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nitawapumzisha.” Jibu lako lingekuwa nini katika uamuzi huo? Jibu lako lingekuwa nini? Mungu anafanya kongamano pamoja nawe sasa hivi.

¹²⁴ Vipi kukuhusu wewe, mwanamume mgonjwa, ama mwanamke? Mungu anafanya kongamano pamoja nawe. “Je, utanipokea? Utaamini Neno Langu? Unaniona katika nguvu na matendo, unanisikia Mimi nikinena kupitia midomo hii inayokufa ya wanaume na wanawake, ambao wameyasalimisha maisha yao Kwangu, nami niliahidi nilipopaa Juu, nitawapa wanadamu vipawa.” Aliahidi jambo hilo. “Mnaona Neno Langu likitimizwa, kama nikilitimiza hilo, ninatimiza Neno Langu lote.”

¹²⁵ Kongamano linafanywa sasa hivi, analifanya pamoja nawe. Huna budi kufanya uamuzi, Mungu anangojea jibu lako. “Nitakutumikia Wewe, Bwana. Ninataka Roho Mtakatifu.” Ama, “Simtaki, sitampokea, mwondolee mbali.” “Ninaamini uliniponya, Bwana.”

¹²⁶ Mungu anangojea kusikia uamuzi wako ni upi. Wewe ndiwe unayepaswa kuufanya, Yeye tayari amefanya Wake, Yeye amethibitisha ya kwamba alifanya Wake. Sasa huna budi kufanya wako, sina budi kufanya wangu, kanisa hili halina budi kufanya wake, sote hatuna budi kufanya uamuzi wetu. Utafanya nini juu yake?

¹²⁷ Gethsemane, kisha kifo Chake, kuzikwa, kufufuka. Kulikuwako na kongamano lingine lililofanywa, hebu tuliendee upesi kwenye makongamano haya. Tutafunga katika dakika moja. Kulikuwa na kongamano la Kipentekoste lililofanywa wakati mmoja. Watu waliokuwa wametembea pamoja na Yesu, na kumsikia Yeye akinena juu ya baraka, na, loo, akaahidi kwamba kuja kwa mamlaka, Mungu aliwaambia kabla hajaondoka duniani, akasema, “Acheni kuhubiri, msiimbe nyimbo zingine, hebu tusifanye jambo lingine lolote sasa, ninawatakeni mwende huko kwenye mji wa Yerusalemu, nami ninawatakeni mngojee huko, kwa sababu tutakuwa na kongamano Utukufuni. Baba, pamoja nami, na Malaika wote tutakuwa na kongamano, nasi tutafanya uamuzi. Ninyi ngojeni huko juu, Tutawaambia jinsi Kanisa litakavyoendeshwa.”

¹²⁸ Ninaweza kuwasikia mitume wakisema, “Vema, labda tutakuwa na maaskofu na makuhani wakuu, na tutakuwa na mambo haya yote, mwajua. Kwa hiyo, tutapanda tu na kungojea tuone uamuzi ni upi. Tutaona kama tunapaswa kuunda madhehebu, kama askofu atayaongoza, ama papa atayaongoza, ama kama mtu fulani mashuhuri atayaongoza, tutaona ni

nani atakayemchagua. Sijui kama mimi nitakuwa ndiye huyo kiongozi.”

“Sijui kama mimi nitakuwa huyo kiongozi.”

Huyo mwingine akasema, “Nitakuwa juu ya hayo yote.”

“Vema, Yeye alinibariki. Aligemea begani mwangu. Alifanya *hivi*.”

¹²⁹ Loo, jamani! Iliwachukua siku kumi kujiandaa kwa ajili yake, wakati walipokuwa wakingojea hili, ndipo wote wakaungana kwa nia moja. Hivyo ndivyo tunavyofanya usiku wa leo. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya kwenye kongamano hili. Ninyi Wamethodisti wote, Wabaptisti, Wapresbiteri, Walutheri, Wakatoliki, na chochote ulicho, sote tunapaswa kuwa katika nia moja, tukungojea kusikia hiyo taarifa rasmi. Na baada ya . . .

¹³⁰ Mahali pazuri sana ambapo lingeweza kutatuliwa palikuwa ni Utukufuni. Mungu alishuka, nalo kongamano likafanywa, jinsi ambavyo Kanisa halina budi kuendeshwa. Je, linapaswa kuongozwa na maaskofu, na madhehebu, na mitambo fulani? Linapaswa kuendeshwaje? Nao wote walikuwa mia na ishirini katika chumba cha juu wakingojea.

¹³¹ Vema, taarifa rasmi ikaja: “Na ghafla akaja kasisi mmoja barabarani, ukosi wake umepinduliwa upande wa nyuma, “Toa ulimi wako na upokee ekaristi takatifu.”

Hilo linasikika la kipumbavu.

“Loo, la, hilo ni kosa. Askofu akashuka, na kusema, ‘Sasa ngojeni kidogo, hatuwezi kuvumilia mambo haya.’”

La, la.

¹³² “Lakini kwa ghafla kukaja kutoka Mbinguni uvumi kama upepo wa nguvu ukienda kasi.” Si mchungaji kusema, “Nipe mkono wa kuume wa ushirika, tutakujaribu kwa miezi sita.” La, bwana. “Kukaja sauti,” si kutoka kwenye seminari, bali, “kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.” Ndipo ile Nguzo kubwa ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, Israeli ya kale, kupitia Israeli ikajigawa na Ndimi za Moto zikakaa juu ya kila mmoja wao, Mungu akijigawa Mwenyewe Kanisani, *mmoja* kuwa nabii, *mmoja* kuwa mtume, *mmoja* kunena kwa lugha, huyo *mwingine* kufanya jambo lingine, Mungu akijigawa Mwenyewe.

¹³³ Mungu mmoja alifanya kazi katika ofisi tatu, Mungu mmoja aliyeitwa Ubaba; Mungu yeye yule aliishi ndani ya Mtu aliyeitwa Yesu, akaitwa Mwana; sasa Yeye yuko katika Kanisa Lake, akiitwa Roho Mtakatifu, alijigawa Mwenyewe katika Mwili Wake wa ulimwengu mzima. Haleluya! Mwili wa kisiri wa Yesu Kristo uliozaliwa kwa Roho wa Mungu!

134 Kwa hiyo kama ilivyosemwa na, na ndugu yetu rabi, asubuhi ya leo, mpendwa wetu, kuhusu umoja pamoja, hatujagawanyika. Ibilisi hujaribu kutugawanya kwa vyombo vyake vya mitambo, kwa kusema, “Mimi ni mfuasi wa Assemblies. Mimi ni mfuasi wa Umoja. Mimi ni mfuasi wa *hili*. Mimi ni mfuasi wa *lile*.” Lakini hatujagawanyika. Mungu huwapa Roho Mtakatifu wale wanaomtii Yeye, na pande zote mbili zimempokea Roho Mtakatifu. Ni nani waliomtii? “Hatujagawanyika, sisi sote ni Mwili mmoja.” Hilo ndilo kusudi letu la kongamano. Hatujagawanyika, sisi ni Mwili mmoja.

135 Roho Mtakatifu, Mungu akijigawa Mwenyewe, akifanya wana na binti, ikiketi juu yao, ile Nguzo ya Moto ilijigawa Yenyewe, “Na Ulimi wa Moto ukakaa juu ya kila mmoja wao. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha zingine, kama Roho wa Mungu alivyowajalia kutamka.”

136 Kulikuwako Yerusalemu maaskofu wakikaa, maaskofu wakuu, mapapa, na kadhalika, watu mashuhuri, mataifa yote chini ya Mbingu, basi wakati ushauri ulipokutana, nao wakasema, “Mbona, watu hawa wote wamelewa kwa mvinyo mpya.”

137 Petro alisimama katikati yao, akasema, “Hawa hawajalewa, kama mnavyodhanja wamelewa, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana. Lakini hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli,” Yoeli 2:28, “‘katika siku za mwisho, asema,’” siku za mwisho wingi, siku mbili, miaka elfu mbili iliyopita, “‘asema Mungu, “Nitawamwagia watu wote Roho Yangu,”” Myahudi, Mmataifa, Myunani, mfungwa au mtu huru, mwanamume au mwanamke, “‘Nitawamwagia watu wote Roho Yangu, nao watatabiri, wana na binti Zangu. Nitaonyesha ishara katika mbingu juu na katika nchi chini, Nguzo za Moto na mvuke wa moshi.””

138 Kasema, “Hebu niwaambie waziwazi juu ya mzee wetu Daudi, kwa kuwa Daudi alisema, ‘BWANA alimwambia Bwana wangu, “Keti mkono wangu wa kuume, nitawafanya adui, kibao cha kuwekea miguu.” Isitoshe, mwili wangu utakaa katika tumaini kwa sababu hutaiacha nafsi yangu katika kuzimu; wala hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu.’

139 “Hebu niwaambie juu ya mzee wetu Daudi, kwa kuwa amekufa na kuzikwa, na kaburi lake liko kwetu leo. Daudi amekufa na kuzikwa pia,” ndipo akawaambia yale waliyokuwa wamefanya. Lakini kasema, “Yesu yuyu huyu, ambaye mmemsulubisha kwa mikono ya watu wabaya, Mungu amemfanya Bwana na Kristo pia.” Amina.

140 Samahani. Sikumaanisha kutembea huku na huku, labda Kitu fulani kilikuwa kikinifanya nitembee. Kwa vyovyote vile, nimevaa viatu vyangu vya kutembea. Loo, jamani! Ninataka kufanya safari siku moja kama Henoko na kupanda juu moja kwa moja.

¹⁴¹ Huku wamesimama katika kanisa la Ndugu Outlaw si muda mrefu uliopita huko Phoenix, Arizona, walikuwa wakiimba wimbo, “Tunapanda juu, juu; juu, juu, juu.” Baada ya kitambo kidogo nikafikiri nimeondoka. Kasema, “Raundi ya kwanza,” kupanda ngazi, kasema, “Raundi ya kwanza ilikuwa ni kuhesabiwa haki; raundi ya pili, utakaso; raundi ya tatu, kutukuzwa; ndipo Roho Mtakatifu akashuka. Nikaanza kupanda juu, juu; juu, juu, juu; juu, juu, juu; juu, juu, juu mpaka nikaifikia ile Njia ya Kilimia Cheupe.”

¹⁴² Nikawazia, “Tukipanda juu zaidi, tutaondoka moja kwa moja kutoka humu kanisani!” Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi ni kuifikia ile Njia ya Kilimia Cheupe hadi Kalvari, tuinuke katika nguvu za Roho Mtakatifu, tuweke kando kanuni zetu za imani na tofauti zetu, tuanze kwenda juu, juu; juu, juu, juu. Hilo ndilo tunalohitaji kufanya, kupanda juu.

¹⁴³ Hilo lilikuwa ni kongamano la Kipentekoste. Walianza kuhubiri uponyaji wa Kiungu, nguvu za Roho Mtakatifu. Petro aliwaambia la kufanya kwenye Siku ya Pentekoste, kasema, “Tubuni, kila mmoja wenu.”

Wakasema, “Tufanyeje tupate kupokea huu? Tunawezaje kuokolewa?”

¹⁴⁴ Petro akasema, “Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa kizazi hiki, na ni hivyo tu, siku za miujiza zitakoma.” Hilo huenda likawa katika *Shajara Ya Siku Ya Kuzaliwa Kwa Kina Mama*, lakini hiyo si Biblia ya Mungu kulingana na Matendo 2. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁵ Yeye alisema, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Huo ni uamuzi wa Mungu, hilo ni kongamano Lake.

Walipokuwa wakisema, “Tutafanya nini?”

¹⁴⁶ Loo, akili za Kanisa na nguvu za Mungu zikakutana pamoja. Nguvu za Mungu zikasema, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Na maadamu Yeye angali anaita, uamuzi Wake wa kongamano ungali unatimiza kila sharti, Yeye ataimwaga Roho Yake. Maadamu Mungu angali anawaita wenye dhambi watubu, Yeye ana Roho Mtakatifu wa kumimina ndani yao.

¹⁴⁷ “Ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu. Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Loo, jamani! “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona,” yaangalie

hayo makongamano, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata mwisho wa ulimwengu.” Ni kongamano la jinsi gani!

¹⁴⁸ Ndipo wakatoka, Petro na Yohana, wasio na elimu wala maarifa. Ninaweza kuthibitisha walikuwa Wapentekoste, walikuwa wamepata baraka za Kipentekoste, kwa njia nyingine, hawakuwa na pesa zozote. Wakaenda kwenye mlango ulioitwa Mzuri, na hapo alilala mtu mmoja, kiwete tangu tumboni mwa mama yake, nao wakasema... akainua kikombe chake kidogo apate sadaka. Akaangalia kule aone kama huyu, jamaa hawa walionekana kama waungwana, huenda wakampa kitu fulani.

¹⁴⁹ Sasa, hiki hapa kinachothibitisha walikuwa Wapentekoste, kasema, “Sina fedha wala dhahabu, bali nilicho nacho!”

¹⁵⁰ Loo, ndugu, chukua fedha yako na dhahabu unipe *hilo*; chukua theolojia yako yote ya seminari unipe *hilo*; chukua elimu yako yote na mambo yako yote makuu unipe *hilo*, kwa kuwa *hilo* tu ndilo litakalokupeleka juu, juu; juu, juu, juu.

¹⁵¹ Fanyeni kongamano, Mungu alisema mngeweza kulifanya, “Atakaye na aje.” Kupanda juu.

¹⁵² “Nilicho nacho, nakupa wewe,” imani. “Katika Jina la Yesu Kristo, simama uende.”

¹⁵³ Hakushangaa juu yake, alinyosha mkono akamnyanyua na kumshikilia pale mpaka vifundo vyake vya miguu vikaanza kupata nguvu kidogo, nguvu kidogo. Hapa akaanza kutembea, kisha akaanza kukimbia, halafu akaanza kurukaruka. Yeye alikuwa Mpentekoste, pia, basi, naam, alikuwa mtakatifu-anayeruka. Naye akashuka kupitia pale akiruka tu, na kuchechemea, na kumsifu Mungu. Kama hiyo si Pentekoste, sijawahi kuona moja.

¹⁵⁴ Ninaweza kuwathibitishia ya kwamba Israeli walikuwa ni Wapentekoste. Waliposhinda na kuona wanyapara, kama vile ulivyoshinda, ukaona wiski, sigara, na vitu vingine vyote vikiwa nyuma yako, vimekufa katika bahari nyekundu ya Damu ya Yesu, mnajua kilichotukia? Musa aliimba katika Roho, Miriamu akapiga tari, na mabinti wote wa Israeli wakipiga tari, wakakimbia huku na huku ukingoni wakicheza katika Roho. Kama huo si mkutano wa Kipentekoste, sijui mmoja ulivyo.

¹⁵⁵ Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Ndugu Branham, unahubiri aina hii *mpya* ya wokovu, sivyo?”

Nikasema, “La, bwana.”

Kasema, “Huna baadhi ya wokovu huu *mpya*?”

Nikasema, “La, nina kisa *kipya* cha wokovu *wa kale*.” Hiyo ni kweli. Nikasema, “Huu ndio wa zamani sana uliopo.”

Kasema, “Ulifanywa lini?”

Nikasema, “Kabla ulimwengu haujaumbwa kamwe.”

Kasema, “Unafikaje huko?”

¹⁵⁶ Nikasema, “Ayubu 7:27 ilisema, ‘Ulikuwa wapi nilipouweka msingi wa ulimwengu, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha?’”

¹⁵⁷ Vema, dini hii ya kale, ya moyoni, ya anga ya bluu, inayoua dhambi, ikipaza sauti, mbona, jamani, ni ya kale kuliko Biblia, ni ya kale kuliko vilima, ni ya kale—ya kale kuliko dunia. Si mpya, ni kitu cha kale, ni kwamba tu ni kisa kipya. Usichanjwe *utoke* kwake, *njoo* kwake.

¹⁵⁸ Kwa hiyo basi, walikuwa tu kama, kwa kawaida, mnakuta magazeti yote yakianza kuikosoa ama chochote kile, na—na wakawakokota mbele ya Baraza la Wazee, nao wakafanya kongamano, ulimwengu ulikuwa na kongamano, kama lile la Geneva, kadhalika, wakasema, “Tutawafanyaje watu hawa?”

¹⁵⁹ Kasema, “Wanaweza kutoka na kwenda kuhubiri, lakini msithubutu kulitaja jina hilo Yesu. Msihubiri tena katika jina hilo.” Wakawapiga na kuwatisha, kasema, “Kama tukiwasikia mkimtaja Yesu tena, tutawafanyia jambo baya sana.”

¹⁶⁰ Petro na Yohana wakatoka gerezani asubuhi hiyo, kutoka kwenye lile kongamano, nao wakaenda kule, na kusema, “Mnajua nini? Ninaamini afadhali tuitishe kongamano.”

¹⁶¹ Kwa hiyo walikuwa wakitaka kufanya kongamano lingine, sasa, hebu tuliite Kongamano la Matendo 4. Katika Matendo 4 wote walikusanyika pamoja, nao walikuwa wakisimulia matukio mbalimbali, nao wakaitisha kongamano, nao wakapiga magoti, na kuitisha kongamano. Walitaka kumwita Mungu kuuliza kile wangeweza kufanya. Je, wanapaswa kurudi nyuma, ama wanapaswa, au, wanapaswa kufanya nini? Je, wanapaswa kuhubiri uponyaji wa Kiungu? Je, wanapaswa kupatana? Wafanye nini?

¹⁶² Nao wakaanza kuomba namna hii, wote kwa moyo mmoja, mkutano mwingine wa Kipentekoste. Wote kwa nia moja, ninawazia hiyo ilikuwa ni kelele. Hivi hamwazii hivyo? Kila mtu akisema, “Kwa nini makafiri wanafanya ghasia? Kwa nini watu wanawazia ubatili? Hakika, wanaunyosha wa Mwanao Mtakatifu, Yesu, mkono Wake kuwaponya wagonjwa.” Ndipo wakati kongamano hilo lilipoanza kufanywa, nao wakaanza kumwita Mungu, taarifa rasmi ikaja.

“Jamani, labda afadhali muwe waangalifu, huenda mkafungwa gerezani. Afadhali mtulie.”

Mlisikia yale Roho aliyomwambia mmishenari huyo muda mfupi uliopita? “Hakuna kujibweteka.”

Je, yanipasa nipelekwe Nyumbani Mbinguni
Kwa kitanda cha maua ya starehe,
Wakati wengine walipigana wapate kushinda
tuzo,
Na kusafiri kupitia bahari zilizojaa damu?

¹⁶³ Tunatarajia nini? Kupelekwa nyumbani kwa kikapu cha maua? Hebu nipige vita, hebu nionyeshe makovu fulani.

¹⁶⁴ Nilipokuwa nikisoma makala fulani, ama, kitabu kidogo cha mshairi, kilisema ya kwamba Kaisari alikuwa anaenda kuagiza, naye alikuwa anaenda kupanda gari kubwa la farasi, naye alitaka baadhi ya askari wake, askari mwenye heshima apande pamoja naye kupitia kwenye mitaa ya yubile hii kuu. Basi mashujaa wote wakatengeneza manyoya yao, na kupamba ngao zao na chapeo zao, wakijiandaa kupita karibu na Kaisari, na, wakakaguliwe ionekane ni nani angemchagua apande pamoja naye katika gwaride hili kuu, basi kasema mashujaa wake wote walitembea kikamilifu, moja kwa moja, wakapitia hapo, na kusimama na salamu zao.

¹⁶⁵ Basi kasema kote kote Kaisari alimkagua kila mmoja wakati akipita. Kasema baada ya kitambo kidogo maskini askari mdogo, aliyelemaa kwenye mikono yake, aliyejaa makovu usoni mwake mwote, na kadhalika, alipita, naye akajionea aibu, na kidogo akainamisha kichwa chake, akaanza kuondoka, Kaisari akasema, “Ngoja kidogo. Ngoja kidogo hapo! Rudi hapa.”

Maskini yule askari akaja na kupiga magoti, na akasema, “Naam, Mfalme mkuu?”

Kasema, “Ulipata wapi makovu hayo? Ni ya nini makovu hayo yote?”

Akasema, “Niliyapata kwenye uwanja wa vita, nikimpigania Mfalme wangu.”

Akasema, “Wewe keti hapa karibu nami, umestahili ziara hii.”

¹⁶⁶ Sijali kama mimi ni D.D., Ph.D., ama L. maradufu D. Nataka makovu kadhaa kuonyesha ya kwamba nimekuwa vitani. Hivyo ndivyo Wakristo wanavyopaswa kufanya, kamwe usichague mambo rahisi, ya starehe.

Nitashika njia pamoja na wachache wa Bwana
waliodharauliwa,

Nimeanza na Yesu, Ee Bwana, nipitishe.

¹⁶⁷ Karibu miaka thelathini hudumani sasa, nimeenda mbali sana siwezi kurudi nyuma, nataka kuendelea mbele. Hata mwisho uweje, hayo yako mikononi mwa Mungu.

¹⁶⁸ Walikuwa na kongamano, na walipomaliza kuomba, Biblia ilisema lile jengo kweli lilitikisika mahali walipokuwa wamekusanyika pamoja, nao wakahubiri Neno la Mungu kwa ujasiri.

¹⁶⁹ Sasa kongamano moja zaidi, tutafunga. Hilo ndilo kongamano...Huenda hukuhudhuria Kongamano la Geneva, huenda hukuhudhuria mojawapo ya makongamano haya tuliyozungumzia, lakini hili hapa moja utakalohudhuria, hilo ni ile Hukumu. Utahudhuria Kongamano la Hukumu, itakubidi

kuhudhuria hilo. Kama uko tayari, ama kama hauko tayari, hilo ni kongamano ambalo sote tunalijia, kwa sababu Biblia ilisema, “Watu waliwekewa kufa mara moja, baada ya kufa, ile Hukumu.”

¹⁷⁰ Nasi kila mmoja wetu anaelekea huko, kwa hiyo afadhali upate rehema kabla hujaanza, ili iweze kuwa, maana Siku hiyo itakuwa imechelewa sana, huwezi kupata rehema wakati huo. Litakuwa ni ko—kongamano la hukumu, na kila mtu atakuwepo kuwajibika kwa matendo ambayo umefanya katika maisha haya. Nawe utakuwa huko kwa hakika tu kama vile Mungu alivyoandika Biblia, kama vile Mungu alivyoziumba Mbingu na nchi.

¹⁷¹ Enyi marafiki, kwa hakika kadiri tulivyo katika jengo hili usiku wa leo, na hakika zaidi, mtahudhuria kongamano hilo. Nanyi mtaomba rehema, bali hamtapokea rehema, hii ndiyo siku ambayo mnapokea rehema. Lakini wakati utakuja ndipo kwenye hilo kongamano utahukumiwa, si kwa rehema, bali na Mungu mwenye hasira, katika hasira Yake. “Basi kama mwenye haki akiokoka kwa shida, mwenye dhambi na asiyemcha Mungu ataonekana wapi?”

¹⁷² Hebu niwaonyeshe jinsi tulivyo karibu na hilo Kongamano la Hukumu. Mliona? Katika lile kongamano lingine, ninataka kulizungumzia kwa sekunde moja tu, niligusia tu kwa kifupi, walikuwa na kongamano hapa hivi majuzi, sijui kama mnajua hilo ama hamjui. Kile ninii...Watu wengine, sisi—sisi—sisi ambao tunawasiliana na Mungu, nafikiri tunapaswa kuwaangazia watu wetu yale yanayoendelea.

¹⁷³ Hivi mnakumbuka lile kongamano walilokuwa nalo hivi majuzi ambapo Khrushchev alivua kiatu chake kwa nguvu na kukigongesha kwenye...? Mlipata hilo, hilo lilikuwa ni nini? Mnaona? Kumbukeni, kulikuwako na mataifa matano ya mashariki, ya kikomunisti yaliyowakilishwa humo, na mataifa matano huru ya magharibi yaliyowakilishwa humo.

¹⁷⁴ Angalieni, Danieli aliona ono, kile kichwa cha dhahabu kilikuwa Babeli, angalia jinsi hilo lilivyoshuka, angalia, chukua historia katika Biblia. Na kilichofuata kilikuwa ni ki—kifua *hapa* cha fedha, Wamedi na Waajemi, iliyofuata ilikuwa ni shaba. Kila wakati ilizidi kuwa ngumu, nalo lilionyesha ya kwamba ile sanamu ya Mataifa isingeweza kusimama kwa sababu dhahabu ndiyo nzito kuliko zote, na ilikuwa nzito juu, isingeweza kusimama. Na kila wakati kutoka... Dhahabu ilikuwa ndiyo laini kuliko zote, halafu fedha inafuata, na halafu inayofuata ni shaba, kisha chuma ikafuata. Kila mmoja wa falme hizo umefuata mwingine, jinsi hasa Biblia ilivyo sema zingefuatana.

¹⁷⁵ Basi angalieni, yeye alisema basi katika wakati wa mwisho, kabla lile jiwe halijachongwa mlimani, ile sanamu ilikuwa

na vidole kumi vya miguu. Sasa, hivyo vingekuwa vitano kwa kila mguu, vidole viwili vikubwa, vinne, na hivyo vitano vikisimama pamoja. Na kadiri ulivyoona ya kuwa imechanganywa na chuma na udongo, sasa kumbukeni, huo ulikuwa ni ufalme wa Mataifa, mtu yeyote anajua hilo, kwamba ulikuwa wa chuma na udongo, havingeweza kuchanganyikana, kadiri chuma na udongo visivyochanganyikana, wala na hawa hawatachanganyikana, ama kushikana pamoja, hawawezi kupatana.

¹⁷⁶ Sasa, mliona? Mlijua maana ya jina *Khrushchev* huko Urusi? “Uchafu au udongo.” Yeye alikuwa ninii, aliongoza *hizo* falme. Mnajua maana ya *Eisenhower*, kichwa cha *huu*? “Chuma.” Chuma na udongo, wala havingeweza kuchanganyikana. Alinyakua kiatu chake na kukigongesha kwenye... Hakuna kuchanganyikana, hawawezi kuchanganyikana, hawatashikana.

¹⁷⁷ Mnaona marafiki? Kinachofuata kilichosalia ni lile jiwe litakalochongwa, kule Kuja kwa Bwana, kubingirika katika sanamu hii na kuivunja vipande-vipande, na falme hizi zote zitasagwa, na kupeperushwa kama makapi kwenye sakafu ya kupepetea wakati wa kiangazi. Tuko katika wakati wa mwisho, ndugu, dada. Hivi hamwezi kuona mahali tulipo?

¹⁷⁸ Sikilizeni, BWANA ASEMA HIVI: Tubuni. Ninabashiri mapazia matatu, katika Jina la Bwana, kuna moja linaloitwa pazia la chuma, ambalo litakuwa Urusi; angalieni Uchina mwekundu, hilo litakuwa ni pazia la mianzi; ni wa kuchukiza sana, lakini angalieni pazia hilo la zambarau linalojitokeza Marekani na kote ulimwenguni, Himaya ya Kirumi, iliyo katili kuliko zote.

¹⁷⁹ Kumbukeni, katika Jina la Bwana: Tokeni kwake! Tokeni kwenye chochote kinachoambatana nalo, kimbilieni Mwamba, kwa maana Kuja kwa Bwana kumekaribia. Tunahitaji kongamano. Ninahitaji kongamano kuzungumzia mambo haya pamoja na Mungu. Kanisa liko kwenye mwisho wa safari Yake.

Na tuombe.

¹⁸⁰ Bwana, Ee Mungu, tunajua kule kuja kumekaribia. Hapa pamekuwa mahali pazuri sana moyoni mwangu, Shreveport, Bwana. Ni—ninakushukuru tu kwa ajili ya mlango huu mdogo uliofunguliwa, bado; kwa ajili ya taifa, bado kuna majaliwa tuliyo nayo ya milango hii iliyofunguliwa, hakuna askari wanaokuja kutukamata, na kutupeleka hapa nje na kutupondaponda mtaani, bali haitachukua muda mfrefu, Baba, tunaona mambo haya yote yakitendeka.

¹⁸¹ Loo, hebu na tujiandae sasa, Baba. Hebu tukanunue Mafuta huku kukiweko na ya kuuza, si kuuza, bali kupokea tu. Ninaomba ya kwamba utawabariki watu Wako usiku wa leo, bariki ujumbe huu mdogo, uliovunjika-vunjika, na uwape

utukufu watu Wako. Ninaomba haya, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁸² Hebu tuone, sijui kuhusu kadi za maombi. Sininii. . . Yuko wapi Billy Paul? Hakuna kadi za maombi. Vema, mnaamini, hata hivyo? U—unaamini kwa moyo wako wote? Nilitaka kuhubiri jambo hili, usiku wa leo. Labda atagawa kadi za maombi kesho usiku. Walilipa jina, lakini nawaambia kilichosababisha hilo, nilikuwa—nilikuwa nimevunjika moyo sana.

¹⁸³ Ni wangapi wanaojua ya kwamba maono karibu yakuue. Yesu, mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, nguvu zikamtoka. Mnajua hilo? Huyu hapa maskini Bibi Schrader hapa, nilikuwa nikizungumza naye leo mle ndani. Mnashangaa ni kwa nini anakaa namna hiyo? Yeye ana karama ya unabii, hiyo ndiyo inayosababisha hilo.

¹⁸⁴ Danieli aliona ono, akafadhaika kichwani mwake kwa siku nyingi. Watu hawatambui hiyo ni nini. Mnaona? Wewe. . . Lakini Mungu angali hapa. Mungu anajua yote kulihusu. Haikubidi—haikubidi kuja hapa na kadi ya maombi. Ninamhisi Roho Mtakatifu sasa hivi, ninahisi baraka Zake na utukufu Wake.

¹⁸⁵ Ni wangapi huko nje wanaoteseka na ni wahitaji? Inueni mikono yenu. Wanaojua ya kwamba siwajui. Sijui kama ninaweza kuwapata ninyi nyote kabisa, au la. Ninyi ombeni.

¹⁸⁶ Sikilizeni, kuwajulisha tunapozungumza leo, mnakumbuka? Kwa kweli kuna jamii tatu za watu ulimwenguni. Tunajua hilo, siyo? Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Hiyo ni kweli kabisa. Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

¹⁸⁷ Mnamkumbuka Petro kwenye Siku ya Pentekoste? Alikuwa na funguo. Mnaamini hilo? Yesu alisema hivyo. Naye akaufungua Ufalme kwa Wayahudi kwenye Pentekoste, naye Filipo akashuka kwenda Samaria, akawabatiza wote, bali hata hivyo Roho Mtakatifu hakuwashukia. Kwa nini? Walikuwa taifa lingine. Kwa hiyo basi wakaagiza Petro na Yohana waitwe, ambao walishuka wakaja na kuwawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

¹⁸⁸ Kwenye nyumba ya Kornelio, alishurutishwa na Malaika aagizie Petro aitwe. Baada ya hapo, Roho Mtakatifu akawa amefunguliwa kwa kila jamii ya watu wakati huo basi, Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

¹⁸⁹ Kumbukeni, Yesu alipokuwa hapa duniani alionyesha ishara Yake ya Masihi kwa Myahudi, wakaaitambua. Tulikuwa na hilo jana usiku. Mnakumbuka hilo? Akaionyesha Msamaria, wakaaitambua. Lakini hata wakati mmoja hakufanya hivyo mbele ya Mataifa. Kwa nini? Alikuwa na miaka elfu mbili ya Injili. Sasa wakati wenu umewadia, kama vile Wayahudi walivyokuwa na maelfu ya miaka, iliwabidi kuiona, Wa—Wasamaria, na ka—kadhalika, iliwabidi kuiona.

¹⁹⁰ Hawakuwa wakiitazamia... Walikuwa wakimtaazamia Masihi, vema, sisi Wamataifa hatukuwa tukimtarajia, tulikuwa Warumi na makafiri tukibeba rungu mgongoni mwetu, tukiabudu sanamu, hatukuwa tukimtaazamia Masihi yeyote. Masihi huwajia wale wanaomtaazamia. Alijionyesha Mwenyewe Masihi. Na siku hizi Mataifa wanadai wanamtaazamia, bali wanashindwa kumwona. Sasa kama... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹¹ ... alijitangaza Mwenyewe kuwa Masihi kwa mambo aliyotenda, na ninii, kila mwaminio katika Biblia aliyeiona, ambaye alikuwa amekusudiwa Uzima wa Milele, aliamini. Na kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Mungu asiye na kikomo, na ataliruhusu Kanisa la Mataifa liingie katika Ufalme juu ya msingi wao wa theolojia, Yeye angekuwa asiye haki. Bila shaka angekuwa hivyo, maana aliyaruhusu mataifa hayo wamwone. Lakini Yeye aliahidi katika siku hizi za mwisho angetokea, pia.

“Wapi, Ndugu Branham?”

“Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁹² Mnakumbuka yule ndugu akizungumza asubuhi ya leo juu ya kushuka kwa wale Malaika watatu? Wawili wao walishuka wakaingia Sodoma. Daima kuna tatu, iko katika utatu, na utatu ni Mmoja. Mnaona?

¹⁹³ Sasa angalieni, kulikuwako na Wasodoma, Wasodoma wasioamini, walimwengu; kulikuwako na Lutu, Mkristo mwaminio vuguvugu; kulikuwako na Ibrahimu, aliyeitwa atoke kwao, Mteule, Ibrahimu. Mnaamini hilo?

¹⁹⁴ Angalieni, Malaika wawili, wahubiri wa kisasa, walishuka na kuhubiri, hawakufanya miujiza yoyote, ni kuwapofusha tu, na kuhubiriwa kwa Injili kweli humpofusha asiyeamini. Lakini Lutu aliokolewa, bali Ibrahimu aliwakilisha katika, kwa ajili ya siku hii ya mwisho, Kanisa teule, lile Kanisa ambalo mambo ya Kimbinguni yamekuwa yakiingia.

¹⁹⁵ Mwangalieni Malaika huyo, sasa angalieni yale aliyofanya. Sasa, sote tunajua, kupita kosa lolote, ya kwamba Huyu hakuwa ni Malaika, Huyu alikuwa ni Mungu Mwenyewe, ilikuwa ni ile Theofania, Mungu. Ibrahimu alimwita Elohimu, Mungu. Naye alibaki nyuma na kuzungumza na Ibrahimu. Sasa, angalieni ile ishara aliyompa Ibrahimu kwamba ninii... si wakati ulimwengu ulipoangamizwa kwa maji. Kumbukeni wakati ulipoangamizwa kwa maji. Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kula kwao, kunywa, kuoa, na kuolewa, na ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Mnaona? Basi mnaweza kufasiri hilo.

¹⁹⁶ Mwangalieni Malaika huyu wakati alipokuja. Jambo la kwanza alilomwambia Ibrahimu, alikiri kwamba Yeye alikuwa ni Mgeni, watu wawili tu wakiingia. Ibrahimu, akiwa na Roho

wa Mungu ndani yake, alitambua ya kwamba hao walikuwa ni watu wa Mungu, akaingia, akamwambia Sara aandae mkate, huku akienda, akamchinja ndama, na kumwagiza mtumishi amtengeneze, na kumleta. Sasa ngojeni, Huyu alikuwa ni Mungu.

Mtu mmoja aliniambia muda si mrefu uliopita, “Ndugu Branham, usingewazia huyo alikuwa ni Mungu.”

¹⁹⁷ “Ilikuwa ni Mungu, Biblia ilisema alikuwa. Alikula nyama ya ndama, akanywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, na kula ugali wa mahindi, nadhani ndivyo ilivyokuwa, na kula siagi, Mungu Mwenyewe.”

Vema, akasema, “Vema, angewezaje kuwa katika mwili?”

¹⁹⁸ “Unashindwa kujua Mungu ni Nani. Mungu ni Muumba. Umeumbwa kwa kitu gani? Elementi kumi na sita, nurulimwengu, na petroli, na kalisi, na potashi. Vema, Mungu alinyosha tu mkono akachota konzi la udongo, kisha akafanya, ‘*Whiu!* Ingia humo, Gabrieli. *Whiu!* Ingia humo Pakanga. *Whiu!* Mikaeli,’ yeyote yule. ‘*Whiu!*’ Akajilipulia Mwenyewe mmoja. Akashuka akaenda kule akala kisha akatoweka.”

¹⁹⁹ Haleluya! Mwili huu unamaanisha nini? Mungu wangu anaweza kunena, na kama mimi si kijiko kimoja cha majivu, nitafufuka, kwa vyovyote vile.

²⁰⁰ Kama nilivyowaambia mara nyingi, nilikuwa nikichana nywele hizi tatu ama nne nilizobaki nazo, mke wangu akaniambia, kasema, “Billy, unaingia upara kabisa.”

Nikasema, “Sijapoteza hata mmoja wa hizo.”

Akasema, “Naomba, niambie mahali zilipo.”

Nikasema, “Hebu niambie zilipokuwa kabla sijazipata, popote zilipokuwa, ziko huko zikiningojeza niziendee.” Amina. Haleluya!

²⁰¹ Ni kitu gani? Unaoza, “Kila unywele wa kichwa chako umehesabiwa. Nitamfufua katika siku za mwisho.” Haleluya!

²⁰² Mwili wangu ulilazwa katika dunia hii kabla hata hakujakuwako na uhai duniani, kalisi, na petroli, na kadhalika. Mungu ni Mkandarasi, aliweka miili yote chini kana kwamba angefanya mgawo mwingine. Alijua tungekuwa hapa, alijua ningekuwa hapa kabla ya ulimwengu, Yeye alijua ningekuwa nimesimama hapa kabla hapajakuwapo na ulimwengu hapa, alijua ungekuwa umeketi kwenye kiti ulichokalia, Yeye hana kikomo. Bila shaka. Anakujua.

²⁰³ Unaogopa nini? Aliweka jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Biblia ilisema aliweka. Unahofia nini? Una Roho Mtakatifu, umetiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu. Muda gani? “Hata siku ya ukombozi wako.” Amina. Kanisa linaogopa. Msiogope, msihofu, aminini tu, hivyo ndivyo Mungu anavyotaka. Hakika.

²⁰⁴ Nguvu kuu za Mungu, huyo Yehova mkuu akisimama pale katika Thiofania hii, akila nyama, akinywa maziwa, ugali, na—na siagi, na kisha akasema, “Ibrahimu yu wapi Sara, mkeo?”

²⁰⁵ Mwangalie Yeye yule akisema, “Wewe ni Simoni, mwana wa Yona.” Mnaona? Akiwakilisha kile Yeye alichu, Mungu yeye yule. Alikuwa akiishi katika mwili uliozaliwa na bikira wakati huo, sasa Yeye anaishi katika mwili uliozaliwa duniani, bali umetakaswa kwa Damu Yake. Mungu juu yenu, Mungu juu yetu, ile Nguzo ya Moto; Mungu pamoja nasi, katika Mwanawe; Mungu ndani yetu, Roho Mtakatifu. Hakika. Ofisi za Mungu, Mungu yeye yule wakati wote, ofisi mbalimbali. Hakika. Ni Mungu. Mungu, Roho Mtakatifu, Yeye ni Mungu; Yuko pamoja nasi usiku wa leo.

²⁰⁶ Angalieni, Yeye alisema atakuwa katika siku za mwisho kabla ulimwengu haujateketezwa, wakati Kanisa hili la Kipentekoste litakapokuja mamlakani. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za—za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa.” Mwangalie Mungu akidhihirishwa katika mwili pamoja na Sodoma, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Alijua alikuwa ameo, alijua alikuwa na mke, na alijua jina lake lilikuwa Sara.

Naye akasema, “Yuko hemani nyuma Yako.” Kumbuka Biblia ilisema, “nyuma Yake.” Pazia lilikuwa limefungwa, alikuwa hemani.

²⁰⁷ Akasema, “Ibrahimu, Mimi,” kiwakilishi nafsi kingine, mnaona, “Nitakuzuru.” Jamaa huyu alikuwa ni nani? “Nitakuzuru kulingana na ahadi Yangu, na wakati wa uhai. Sara ataninii, wakati huo wa siku ishirini na nane utanza naye tena, atageuka kuwa msichana, nami nitamtembelea.”

Naye Sara ndani ya hema moyoni mwake, hakuna kelele, kasema, “*Humph!*”

Naye huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, kasema, “Kwa nini akacheka?”

²⁰⁸ Ni telepathia ya aina gani hiyo? Ni aina gani ya kusoma akili huko? Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni Mungu katika mwili, naye Yesu alikuwa Mungu katika mwili, na Roho Mtakatifu, usiku wa leo, ni Mungu katika mwili, akilionesha Kanisa, akitimiza ahadi Yake. Utukufu!

²⁰⁹ Loo, enyi Kanisa la Mungu, inukeni kwa mbawa za tai, mkaruke mbali na kitu hiki. Mtachimbaje kwa kina vya kutosha kupita juu yake... mwingie chini yake? Mtajifichaje wakati italipua futi mia moja ardhini, kwa maili mia moja mraba? Vema, huo mtikiso ungepasua moja kwa moja hadi kwenye lava. Lakini kuna njia ya kuepukia, loo, kwenda juu, juu; juu, juu, juu. Hivyo tu. “Nitamfufua katika siku ya mwisho.”

²¹⁰ Enyi wagonjwa, mnaamini ya kwamba Yeye yupo hapa? Na ajiwakilishe Mwenyewe. Sijui. Ombeni, kila mmoja wenu aombe.

²¹¹ Sasa, Bwana, sijui, watu hawa, siwajui, bali kwamba wapate kujua ya kwamba Mungu yeye yule, Mungu yeye yule aliyeishi katika mwili wa mwanadamu kule chini mbele ya Ibrahimu, na wakati alipokuja katika Mwili, uliozaliwa na bikira, akiwa na Damu kuondoa dhambi ya ulimwengu, Dhabihu ya Yehova, Yule aliyekaa ndani Yake, wakati aliposema, “Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu, Yeye anakaa ndani Yangu. Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anakaa ndani Yangu,” Naye alifanya kazi zile zile alizofanya wakati alipoishi katika Mwili huo, akisimama pale mbele ya Ibrahimu, akaahidi kwamba ninii, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

²¹² Nilihubiri Ujumbe mgumu wa *Makongamano*. Tuko kwenye kongamano, tunakuita Wewe, Bwana, Wewe fanya uamuzi. Je, wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Nimejaribu kuhubiri Neno Lako jinsi tu lilivyoandikwa, nimejaribu kusimama juu ya Hilo. Kama Wewe upo hapa, Baba, tupe uamuzi Wako. Je, Wewe ni yeye yule? Uko hapa kutenda katika mwili wetu mapenzi ya Mungu, na kufanya mambo uliyoahidi utafanya? Lithibitisha, Bwana, angalau kwa wawili au watatu katika hili kusanyiko. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²¹³ Asiweko anayesogea, kimya kabisa, wenye kicho kabisa sasa.

²¹⁴ Kama mtu yeyote anataka kuja hapa na kuchukua mahali pangu, kama huamini hii ni kweli, njoo hapa ujaribu. Karibu mimbarani.

²¹⁵ Ni wangapi katika jengo hili hapa ambao ni wagonjwa, na unajua ya kwamba sikujui, sijui lolote kukuhusu, inua mkono wako. Hakuna mtu ninayemjua. Ni wangapi walio na shauku moyoni mwao kwa ajili ya mpendwa fulani, ama kitu fulani? Unajua sikujui. Ama unahitaji chochote, amini tu.

²¹⁶ Mbele za Mungu, mbele za Roho Mtakatifu, nitaangalia na kuona kama ninamjua mtu yeyote katika jengo hili ambaye mimi, kwa kweli, ningemjua. Kuna mtu aliyeketi hapa ambaye ninamwangalia, sijui jina lake, alikuja hapa pamoja na wamishenari hao. Na—nasahau jina lako. Nilitambulishwa kwake hivi majuzi.

²¹⁷ Mtu huyu hapa hunipungia mkono mara kwa mara, bali simjui, sijui yeye ni nani. Ninatazama tu niwe na hakika ya kwamba mimi... Ninamjua Dada Schrader aliyeketi hapa, bila shaka, Jackie, binti ya Ndugu Moore, na huyo hapo binti-mkwe wangu, Loyce. Na huyu si ni yule mama hapa kutoka huko Hot Springs ambaye nilizungumza naye asubuhi ya leo, Dada Humbard? Naam. Wasemaje? Humbard. Ninamjua. Nje ya hao simjui mtu yeyote huko nje. Nitalishika jukwaa, labda kesho usiku, Bwana akipenda.

²¹⁸ Vema, hebu tuone, Biblia ilisema, “Nijaribuni, asema Bwana.” Hiyo ni kweli? Sasa, iweni waaminifu na mwombe,

hebu nigeuze mgongo wangu mwone kama Mungu hutimiza Neno Lake. Ikiwa Mungu aliyeishi katika mwili huo kule chini wa Mtu huyo, Theofania hiyo, ama chochote kilichokuwa, Mungu aliyekaa ndani ya Yesu Kristo, ambaye Yesu... Kila mtu alidhani alizungumza maradufu, lakini wakati mwingine ilikuwa ni Yeye akinena, wakati mwingine ilikuwa ni Roho akinena.

²¹⁹ Sasa, kumbukeni Yesu alikuwa Mungu, sisi si Mungu. Alikuwa na Roho bila kipimo, “Utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake,” bali sisi tunaye Roho kwa kipimo. Vema sasa, kama ningechota kijiko kimoja cha maji kutoka baharini, hiyo ingekuwa ni kulinganisha, kamwe usingekosa jambo hilo. Vema, huyo ni Roho Mtakatifu aliye juu yangu na juu yako. Lakini kumbukeni kama mimi... Naye Yesu alikuwa na bahari hiyo yote, ilikuwa ndani Yake, yote.

²²⁰ Lakini kama ningechota kijiko kimoja cha maji kutoka baharini, kemikali zile zile zilizo katika bahari nzima zimo kwenye kijiko hi—hicho, kila kemikali baharini iko mle ndani, iko kwenye maji. Ni Roho yeye yule, bali si mwingi hivyo, bali atatenda vivyo hivyo, maana Yeye aliahidi jambo hilo.

²²¹ Ninawaomba tu msemi hivi: “Bwana,” hakikisha umeweka Andiko, “Imeandikwa katika Maandiko ya kwamba Wewe sasa ni Kuhani wetu Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Nina haja. Bwana, uthibitishe Neno Lako kwangu, jalia niweze kugusa vazi lako.”

²²² Laiti... Si—sisemi ya kwamba atafanya hivyo, kumbukeni, sisemi atafanya hivyo, ninaamini tu Neno Lake.

Sasa, kama ungesema, “Ndugu Branham niponye.”

La—laiti ningaliweza. Kama Yesu angekuwa amesimama hapa, asingeweza kufanya hivyo, tayari amelifanya, Yeye anajaribu tu kukufanya uamini.

²²³ Kama atafanya hivi, kwenu ninyi watu huko nje, mkiketi tu huko nje, hivi itaondoa kila shaka, nanyi mtaamini kwa moyo wenu wote, kote jengoni? Je, mtamwinulia Mungu mikono yenu, msemi, “Ingenifanya tu niamini hilo”? Vema, omba.

²²⁴ Sasa, Bwana, hili si la maonyesho, hili ni kuthibitisha Neno Lako. Wewe hutimiza Neno Lako, ninaamini kila moja la Hayo. Sasa, kuna wanaume na wanawake huko nje walio na haja, kama vile watu walivyokuwa siku ulipokuwa duniani, kama yule mwanamke alivyogusa vazi Lako. Uko Utukufuni usiku wa leo, umeketi mkono wa kuume wa Ukuu, Nawe ni Kuhani Mkuu, ulisema, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

²²⁵ Hatuwezi kuponya, tunajua sisi si waponyaji, bali Wewe unajitambulisha Mwenyewe, ya kwamba Wewe ungali ni Mungu. Jalia mtu fulani, Bwana, awe na imani ya kutosha kukugusa Wewe wakati huu. Ninaomba ya kwamba—ya kwamba

utaniruhusu, mtumishi Wako asiyeatahili na asiyeata, niweze kujituliza na kujiondoa mwenyewe njiani, upate kuna siri Zako kwa Kanisa Lako kuthibitisha.

²²⁶ Baba, Musa hakustahili kushuka kwenda Misri, bali Wewe ulimchagua; Petro, yule mvuvi, hakustahili kuwa mtume, bali Wewe ulimchagua. Sisi si mali yetu wenyewe, tumenunuliwa. Mimi sistahili kuwa mtumishi Wako, bali Wewe umechagua, hakuna mmoja wetu anayestahili, bali Wewe umechagua.

²²⁷ Jalia iwe usiku wa leo, Bwana, ambapo ile sehemu ngumu ya Neno Lako itatimizwa, kusudi watu wapate kujua ya kwamba Wewe ni Mungu, nami ninawaambia Kweli. Sasa, watu wanaangalia na wanashangaa, nayo Biblia imesema dhahiri, “Akiwepo mmoja miongoni mwenu, ambaye ni nabii, nitasema naye; yale huyo mtu asemayo ni kweli, yakitimia, basi msikieni.”

²²⁸ Baba, ninasema jambo hili wapate kuamini Ujumbe ninaowahubiria, ninaomba ya kwamba Wewe utathibitisha. Nilina habari Zako, sasa nena, Bwana, ya kwamba nimesema Kweli. Tujalie, Baba, ninapokungojea Wewe kwa ajili ya mvuto wa imani kutoka mahali fulani, katika Jina la Bwana Yesu.

²²⁹ Kuna mama fulani, ninamwona mbele yangu, anaogua yabisi kavu. Huyu hapa ameketi papa hapa, ameinua mkono namna *hii*. Hiyo ni kweli. Ulikuwa ukiomba ya kwamba Mungu angenigeuza, sasa Yeye amenigeuza, yabisi kavu yako imekwisha.

²³⁰ Simjui huyo mama, sijawahi kumwona. Hivi hatufahamiani, mama? Sikujui, hunijui mimi. Kusudi uweze. . . Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Ninamaanisha mtumishi Wake. Neno hilo hukwaza wengi wa . . . Niangalieni, aminini.

²³¹ Vipi kuhusu mvulana huyo? Unaamini Mungu anaweza kuniambia huyo mvulana ana shida gani? Kama ningeweza kumponya, ningemponya. Siwezi, lakini, Yesu hawezi, lakini Mungu yuko katika miili yetu sasa. Mvulana huyo ana homa ya baridi yabisi. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ama, alikuwa nayo, hana sasa.

²³² “Kama anaweza kuamini!” Aligusa nini, huku nimegeuza mgongo wangu? Alingusa Kuhani Mkuu. Unaamini sasa? Mtu fulani aombe, amini, uwe na imani. Kuna wengi wenu, wengi sana.

²³³ Unafikiri ataponywa kansa hiyo? Shangazi yako. Unaamini ya kwamba atapona? Vema. Hayupo hapa, bali ulikuwa ukimwomba, shangazi aliye na kansa. Amini, naye atapona.

Amini tu, usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote. Mungu hujibu maombi. Unaamini hilo? Mwamini Mungu.

Mtu fulani kupitia sehemu hii, mahali fulani, haidhuru uko wapi, omba.

²³⁴ Ee Yehova-Yire, Yehova-Rafa, Mungu wa ono, Mungu mwenye nguvu, Mungu Yule tunayemjua katika Yesu Kristo, na iwe hivyo, Baba. Naam.

²³⁵ Sasa kuona kama ninaweza kumwona mtu huyo. Ninamwalia mtu fulani huko nyuma anayeonekana kuwa karibu. Ted Dudley. Je, huyo ni Ted aliyeketi hapo? Nilidhani ni yeye. Papa hapa ndani, ni Ted? Iko moja kwa moja nyuma yako. Mama fulani huko nyuma, naam, mnaona, yeye siye mgonjwa, anamwomba mwanawe. Hiyo ni kweli. Ni mama mkongwe. Anaishi Mississippi, mwenye dhambi ambaye unamwomba apate kuokoka.

²³⁶ Sijawahi kumwona maishani mwangu. Je, mambo hayo ni kweli, mama? Inua mkono wako. Je, Mungu angali anafanya kazi katika mwili wa mwanadamu? Vipi kuhusu ninyi nyote huko nyuma sehemu hiyo? Mnaamini huko nyuma? Omba kwa moyo wako wote.

²³⁷ Yeye, Yule ajuaye mambo yote, nakuomba Wewe, Bwana, ukijua mioyo ya wanadamu, si kwamba watu wapate kujulikana, kama ulivyonena kwa lugha asubuhi ya leo, lakini Ujumbe huu ulisema kuna manabii katikati. Tunajua huyo ni Wewe, Bwana. Ungezungumza na nani huko nyuma?

²³⁸ Naam, kijana mwanamume, amevaa sha—shati lililofungwa vifungo, hana tai, ni shati la mchezo. Hapa. Sikujui, ewe jamaa mdogo, sijawahi kukuona maishani mwangu. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Umetoka mbali na hapa, kutoka shuleni. Amini. Unamwomba maskini ndugu yako, ana kifafa. Uko Texas wakati huu, lakini maskini ndugu yako anatoka katika nchi iliyo na milima ndani yake, ni Idaho. Jina lako ni Bw. Hunt. Mwamini Bwana Yesu Kristo, na upokee ulichoomba.

²³⁹ Loo, Ua la Uwandani, Yungiyungi la Bondeni, Nyota ya Asubuhi, Alfa, Omega, wa Kwanza na wa Mwisho, Shina na Mzao wa Daudi!

Mtu aliyeketi pale mwenye ngiri maradufu, henia, amefanyiwa upasuaji mara mbili kwa ajili yake. Bw. Finn kutoka Mississippi. Sikujui, lakini huo ndio ukweli.

Unaamini? Amini.

Bi. Farmer, sijawahi kukuona maishani mwangu. Unaamini Mungu anaponya ugonjwa wako wa koo? Unaweza kwenda Mississippi, pia, na upone.

Bi. Boyd, kando yake, unatoka Shreveport, sikujui, lakini una ugonjwa wa bursiti, uvimbe wa neva. Pona.

Ninakupa changamoto kumwamini Bwana. Mimi si Yeye, bali Yeye yupo hapa.

²⁴⁰ Unayepangusa machozi kutoka machoni mwako, umelala kitandani, ukifa. Kulikuwa na wenye ukoma watatu walioketi langoni wakati mmoja, wakasema, “Kwa nini tuketi hapa? Kama

tukiketi hapa, tutakufa kwa njaa.” Huko mjini, walikuwa wakila watoto wao kwa wao. Kasema, “Kwa nini tuketi hapa? Hima twendeni tukafanye jambo fulani kulihusu. Tukienda kwenye kambi ya adui, wakituua, tutakufa, kwa vyovyote vile. Tutakufa, kwa vyovyote vile, lakini labda watatuokoa.” Na kwa msingi wa kwenda kwenye kambi ya adui, Mungu aliwatunukia.

²⁴¹ Kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, mama... Umetiwa uvuli, kuna kivuli cheusi juu yako, unakufa. Kama ataniambia shida yako ni nini, je, utasimama, na usiende kwenye kambi ya adui kubahatisha, bali uje kwenye nyumba ya Mungu aliye hai mahali unapotarajiwa? Utaniamini mimi kama nabii Wake? Una kansa kwenye uti wa mgongo. Umekuwa kitandani kwa majuma kadhaa. Simama, pokea uponyaji wako. Nenda nyumbani katika Jina la Bwana Yesu.

Unaamini? Wangapi...? Huyo hapo! Mgongo uliponywa kansa! Hebu tumsifu Mungu.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya mwenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo kwa... aliyechinjwa;
Mpeni utukufu... (Yale tuliyosema...) 

60-1125 Kongamano
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org